
SportPesa
TZS. 896,686,220
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SABAYA** adai kesi yake ni ya kubambikiwa



BIBI SARA ASIMULIA JIJI MBEYA LILIKOTOKEA... Ukurasa 12

Watanzania tuache kuendekeza masihara haya! Ukurasa 13

BUFE

IJUMAA FEBRUARI 4, 2022 Nipashe MIAKA 60 YA UHURU

MKUU MAGEREZA: SASA TUNAJILISHA 90% Ukurasa 14

Mtaalamu ujasiriamali na darasa la kuendelea kupitia usomaji vitabu

IMEELEZWA kuwa mbinu za kufanikiwa kimaisha ni kuwekeza katika kusoma vitabu mbalimbali. Hapo nafasi ya uelewa kuhusu stadi za ujasiriamali nazo zina nafasi zake.

Kinadharia inaelezwa, pasipo kutumia mbinu na stadi mbalimbali za kujifunza, ni ngumu kwa mtu kubadilika kimaisha, ananena Mkurugenzi Mtendaji katika Taasisi ya Uongozi na Ujasiriamali (IMED), Dk. Donald Olomi, wakati wa uzinduzi wa kitabu kiitwacho 'Anza Kuwa na Stawi'.

Dk. Olomi alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo wa kitabu kilichoandikwa na Prosper Magali, ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wadau wa Nishati Jadilifu Tanzania (TAREA)...

...wanamaliza masomo katika vyuo, lakini hawana ajira rasmi, pia kundi kubwa halipo katika sekta yoyote rasmi.

"Ili kupunguza tatizo la ajira ni lazima kuwasaidia waweze kukua na ustawi," anasema Dk. Olomi, akielimisha hata wafanyabiashara wakubwa wa sasa, walianza na ujasiriamali ngazi ya chini.

Anaongeza kwamba inatakiwa kukuzwa vipaji vyao, ili waweze kunufaika na fursa zilizoko katika jamii zao.

USHUHUDA GEREJI

Rashid Hamza Nzowah, Mkurugenzi...

Nipashe
Ijumaa Februari 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580846
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Kikwete atoa neno utendaji wa Samia

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan

Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete

## CCM yaweka mtegoni vigogo wa halmashauri

**YASHANGAA** kilomita tano kujengwa miaka mitano...*Endelea ukurasa 2*



Rais mpya wa Mastercard Kanda ya Afrika, Mark Elliott, akibonyeza kitufe kuchezesha droo ya tano ya Mastabata Kivyako Vyako, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto), Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi, Filbert Mponzi (wapili kulia) na Meneja Mwandamizi wa Biashara ya Kadi, Manfredy Kayala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 4

## MGOMO WA MABASI ULIVYOITIKISA IRINGA

MADEREVA wa mabasi yanayotoa huduma za usafiri katika mikoa ya nyanda za juu kusini; Njombe, Mbeya na Ruvuma, jana waligoma kutoa huduma wakishinikiza uongozi wa Halmashauri ya...

## Naibu Spika Kujulikana Februari 11

UKURASA 2

MICHEZO YANGA YAITISHA MBEYA CITY FC UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Kikwete atoa neno utendaji wa Samia

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, amewataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi anazozifanya katika kuleta maendeleo kwa nchi na kukiimarisha chama.

Kikwete aliyasema hayo jana alipohutubia kwenye maadhimisho ya Miaka 45 ya CCM Mkoa wa Pwani yaliyofanyika Chalinze wilayani Bagamoyo.

Alisema: "Rais Samia anaonyesha njia kwa kuonyesha tuko wapi na tunaenda wapi, ni mchapakazi na hodari, jasiri katika kuamua na kuchukua hatua.

"Kuna dalili ya mambo makubwa mazuri yanakuja mbele, miezi tisa ya uongozi wa Rais Samia amefanya mambo makubwa ya kustaajabisha. CCM ni ileile, hakuna lililoharibika, ameithibitishia dunia kuhusu ujuzi na maarifa katika uongozi wake."

Kikweta pia aliwataka wanachama wa CCM kutumia vizuri uchaguzi wa ndani ya chama kupata viongozi watakaojenga mshikamano kati ya chama na serikali.

Aliwataka wanachama kuwa makini na kuepuka kuchagua viongozi ambao watakuwa na maslahi binafsi na wale ambao watakuwa chanzo cha mifarakano badala yake kutoa nafasi kwa viongozi waadilifu.

"Tutumie vizuri nafasi ya uchaguzi wa ndani ya chama, tuchague viongozi watakaotutoa hapa kwenda mbele na watakaotusaidia kujenga mshikamano na ushirikiano kwa serikali yetu, tuwakatae watakaosababisha mifarakano.

"Tusiwape nafasi wanaotaka uongozi kwa ajili yao na si kwa manufaa ya wanachama kwani kuna watu wana sababu zao, ama apate uongozi amkomoe fulani, mkiwatambua hao achaneni nao," alitoa hadhari.

Kikwete alisema umakini usipokuwapo kwenye kuchagua viongozi na wakawekwa wenye maslahi yao, watatumia muda mwingi kwa ajili yao hawatakuwa na muda wa kukijenga chama.

Kikwete aliwataka wanachama wa CCM kusikiliza matatizo ya wananchi, pia kuweka mikakati ya kupiga hatua mbele kimaendeleo.

"Mnayo kazi ya kujenga chama ili kiendelee kuwa hai, chama kilicho hai kina viongozi imara wanaotambua wajibu wao kwa uadilifu," alisema.

Awali Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bagamoyo, Abdul Sharifu, alisema ilani imetekelezeka vizuri na kwamba Rais Samia ameifanyia Wilaya ya Bagamoyo mambo makubwa kwenye sekta mbalimbali.

Sharifu alisema Rais asirudi nyuma bali asonge mbele, akiwaomba wananchi wamuunge mkono Mkuu wa Nchi huyo kwa kila hatua.

Mwenyekiti huyo pia alitumia nafasi hiyo kuiomba serikali kufikiria kuipa Chalinze hadhi ya wilaya kwa kuwa ina karibu kila kitu kinachohitajika ikiwamo stendi ya mabasi, hospitali ya wilaya na huduma nyingine nyingi za kijamii.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), Makhtar Sop Diop, baada ya kuwasili Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma jana. Kulia ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula. **PICHA: IKULU**

# Naibu Spika sasa Feb.11

**Na Salome Kitomari**

BUNGE limesema uchaguzi wa Naibu Spika utafanyika Februari 11, mwaka huu.

Kutokana na tangazo hilo, bunge limewataka wanaotaka kuwania nafasi hizo kuwasilisha jina la mgombea kwa Msimamizi wa uchaguzi (Katibu wa Bunge) Februari 10, kabla ya saa 10:00 jioni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge, kila chama cha siasa chenye uwakilishi bungeni kina haki ya kushiriki uchaguzi huo.

"Kwa mujibu wa ibara ya 85 (1) ya Katiba, chama kinachokusudia kushiriki uchaguzi kinaruhusiwa kuanza mchakato wa kumpata mgombea kutoka miongoni mwa wabunge wa chama hicho," ilifafanua taarifa hiyo.

Nafasi ya Naibu Spika inakuwa wazi baada ya Dk. Tulia Ackson kujiuzulu nafasi hiyo Januari 31, mwaka huu, kwa mujibu wa ibara ya 149 (1) (C) na (2) ya Katiba.

Baada ya kuteuliwa na chama chake, aligombea nafasi ya Spika wa Bunge Februari Mosi, mwaka huu na kuchaguliwa kwa kura zotre 376.

Katika kinyang'anyiro hicho Dk. Tulia alikuwa anashindana na wagombea wengine wanane kutoka vyama vya TLP, CCK, ADA-Tadea, SAU, ADC, AAFP na DP.

"Katika mazingira hayo, masharti ya Ibara ya 85 (3) (b) na 86 (2) ya katiba yanaelekeza kufanya uchaguzi kujaza nafasi ya Naibu wa Spika wa Bunge mapema iwezekanavyo mara baada ya kiti cha Naibu Spika kuwa wazi," ilibainisha taarifa hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema bado hawajapokea barua kutoka kwa Katibu wa Bunge na watakapopokea watashauriana kama kuna umuhimu wa kuweka mgombea wa nafasi hiyo.

Kwa mnujibu wa kitabu cha orodha ya wabunge, Bunge hilo linaundwa na wabunge 354 wa CCM, 20 wa Chama cha Demokrasia na Maendelkeo (CHADEMA), Chama cha wanachi CUF watatu, ACT Wazalendo wanne na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

# CCM yaweka mtegoni vigogo wa halmashauri

**Na Beatrice Shayo,** MUSOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema hakijaridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara ikiwamo ujenzi wa barabara ya Musoma-Makojo-Busekera kilomita 92 kwa kiwango cha lami ambayo kwa miaka mitano mkandarasi amejenga kilomita tano na kazi inasuasua.

Mradi wa pili ni ujenzi wa hospitali ya wilaya ambao ulianza mwaka 2019 na mwaka 2021 serikali ilitoa Sh. bilioni 1.49 ili kukamilisha ujenzi huo na hospitali ianze kutoa huduma ifikapo Agosti mwaka 2021 lakini mpaka sasa haujakamilika na fedha ziko kwenye akaunti ya halmashauri hiyo.

Akizungumza katika ziara yake kwenye miradi hiyo juzi, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, alisema ni jambo la kushangaza serikali imetoa fedha ya kukamilisha miradi lakini mpaka sasa haijatekelezwa.

Katika ziara hiyo, Shaka alifuatana na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa mkoani Mara chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, waliozuru mahali huko kwa ajili ya kuangalia utekelezaji wa ilani ya CCM.

Shaka alisema uzembe, urasimu na kukosekana kwa uhusiano na ushirikiano baina ya viongozi na watendaji wa ndani ya halmashauri umechangia ucheleweshaji wa miradi ya maendeleo.

Aliagiza kufanyike ukaguzi maalumu wa miradi yote ya maendeleo katika halmashauri kwa kuwa kuna sintofahamu kubwa katika miradi hiyo.

"Katika hii ziara hata Mkuu wa Wilaya hajaja, ninaagiza miradi yote ya wilaya hiyo ifanyiwe ukaguzi maalumu kwa lengo la kutaka kujiridhisha.

"Nimepatwa na wasiwasi, hatujui miradi mingine ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameleta fedha nyingi ipo katika hali gani.

"CCM hatuwezi kukaa kimya kwa hiki kinachoendelea, mtu aliyepewa dhamana ya uwajibikaji anapaswa awajibike katika sehemu yake ya kazi kwani Rais Samia amewaamini na kama amewaamini lazima kila mmoja atimize imani yake kwa Rais Samia," aliagiza.

Shaka alisema endapo watakwenda kwa mwendo huo, watawakwamisha na chama hakiwezi kukubali uzembe huo wa kukwamisha maendeleo ya wananchi.

Alisema miradi hiyo lazima ifanyiwe ukaguzi maalumu ili wajiiridhishe kama kinachofanyika katika miradi hiyo kina tija na fedha nyingi zilizotolewa na serikali zitaleta matokeo chanya kama inavyotarajiwa.

"Msifikiri kwamba huku hatuwezi kufika, tuna uwezo wa kufika muda wowote ule na ndiyo maana nimekuja, hatuwezi kukubali na tangu mwanzo nimeelezwa hapa hospitali mambo hayaendi na ndicho nilichokikuta hapa," alisema Shaka.

Alisema atapeleka taarifa kwenye kikao cha majumuisho na wataandika taarifa kuhusiana na mwenendo wa miradi hiyo.

"Bahati mbaya hapa DC hayupo ambaye ndiye msimamizi mkuu ambaye anaweza kuchukua maelekezo haya, lakini nitaenda kuelekeza katika majumuisho lazima tujiridhishe hiki kinachofanyika kina tija," alionya.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Musoma, Msogela Palela, alieleza sababu za kutokamilika kwa hospitali hiyo kwa wakati, akisema kuwa ni kukosekana kwa maji na eneo la ujenzi lina mawe mengi.

Hata hivyo, Shaka alipinga sababu hizo kwa kuwa mita chache kutoka mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo kuna Ziwa Victoria.

Shaka alisisitiza kuwa ukwamishaji wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM 2020-2025 ni kuikwamisha CCM na Rais Samia, jambo ambalo chama hakiwezi kukubali.

# Wanafamilia mbaroni tuhuma mauaji

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

JESHI la polisi mkoani Dodoma linawashikilia watu 17, wakiwemo watano wa familia moja kwa tuhuma za mauaji ya kikatili ya watu watano wa familia moja yaliyotokea Januari 22 katika kijiji cha Zanka, Bahi mkoani Dodoma.

Kukamatwa kwa watuhimiwa hao kunatokana na agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alilolitoa Januari 26, mwaka huu, alipotembelea na kuwafariji wafiwa kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Dk. Mpango alitoa siku saba kwa Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi na kuwakamata wahusika wa tukio hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alisema watuhimiwa hao wamekamatwa kutokana na mazingira mbalimbali yaliyohusishwa na mauaji hayo.

Alisema watu hao ndugu watano, wanaume watatu na wanawake wawili, wamekamatwa na simu ya mkononi aina ya TECNO iliyokuwa inamilikiwa na marehemu.

Kamanda Lyanga alisema uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Polisi umebaini watuhimiwa waliwaua watu hao zaidi ya saa 48 kabla ya kujulikana kwa kuwa miili yao ilikuwa inatoa harufu ikiashiria kuharibika.

Alisema sababu zilizobainika hadi vifo vyao ni kuwapo kwa mgogoro wa ndani ya familia na imani za kishirikina, visa vya nyuma kuashiria kulipiza kisasi na kuwapo kwa uhasama wa kibiashara kati ya marehemu na ndugu.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi limetangaza zawadi nono kwa yeyote ambaye atafanikisha kuwakamata wahalifu wengine kuhusiana na tukio hilo la mauaji.

Lyanga alisema msako utaendelea kwa ajili ya kuwatafuta wahalifu hao kuhusiana na tukio hilo, huku akisisitiza ushirikiano baina yao na wananchi.

Alisema lengo ni kuona matukio ya mauaji ya kikatili yanatoweka katika maeneo mbalimbali mkoani Dodoma na kwamba wanaendelea kuwasaka wahalifu wanaofanya matukio ya kikatili katika jamii.



Waziri wa Ujenzi, Prof. Makame Mbarawa (katikati), akimsikiliza Mhandisi Sabyasachi Kar, kuhusu ujenzi wa barabara ya juu katika makutano ya Barabara za Chang'ombe na Nyerere, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sabaya adai kesi dhidi yake ni ya kubambikwa

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai Mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amedai hajashtakiwa na Jamhuri bali kikundi cha watu anaodai walimtengenezea kesi. Sabaya alidai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha alipohojiwa na Mwendesha Mashitaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Richard Jacopiya.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano hayo mahakamani jana:

**WAKILI:** Ni kweli kwamba mbele ya mahakama hii unashtakiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sio kikundi chochote wala mtu binafsi au kikundi cha kisiasa?

**SABAYA:** Sikubaliani na wewe

**WAKILI:** Unashtakiwa na nani?

SABAYA: Na waliotengeneza kesi hii.

(Wakili Jacopiya akaiomba mahakama hati ya mashtaka na kumpatia Sabaya aisome).

**WAKILI:** Soma hapo juu hiyo hati ya mashtaka imeandikwaje?

**SABAYA:** Republic (Jamhuri) dhidi ya Lengai Ole Sabaya na wenzake.

WAKILI: Kwa hiyo hapo ni Jamhuri dhidi ya Lengai Ole Sabaya?

**SABAYA:** Ndio unaniambia hapa kuwa Republic ndo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kwenye hati hii imeandikwa neno Republic tu.

**WAKILI:** Ni wapi wameandikwa kwenye hati ya mashtaka hao waliotengeneza hiyo kesi?

**SABAYA:** Sijaona kama wameandikwa kwenye hati ya mashtaka.

**WAKILI:** Jamhuri ilitoa ushahidi wa mashtaka dhidi yako?

**SABAYA:** Jamhuri haikutoa ushahidi, waliotoa ushahidi ni watu.

**WAKILI**: Kuna kosa lolote mtu kuja kutoa ushahidi mahakamani?

**SABAYA:** Kuna kosa ushahidi wa uongo.

Baadaye Sabaya alihojiwa na Wakili Neema Mbwana. Sehemu ya mahojiano hayo ni hii:

**WAKILI:** Ukiongozwa na Wakili Mahuna, ulisema una ndoa ulioa lini na ulimuoa nani?

**SABAYA:** Nilifunga ndoa tarehe 15 Julai 2018 na nilimuoa Jesca Thomas na ndoa yetu ilifungiwa katika Kanisa la Central Sabath.

**WAKILI:** Umeleta hati yoyote kuthibitisha kuwa umeoa?

**SABAYA:** Kwenye hati ya mashtaka hakuna sehemu inayolalamikia ndoa yangu.

**WAKILI:** Umeleta uthibitisho hapa mahakamani?

SABAYA: Ndio uthibitisho ni mimi hapa mume wake.

**WAKILI:** Umeleta uthibitisho wa maandishi wa cheti hapa mahakamani?

**SABAYA:** Sijaleta lakini mimi ndiye mume wake na ndiyo ushahidi wenyewe.

**WAKILI:** Kwa jinsi ulivyojieleza ulieleza kuwa ulioa ukiwa mteule wa Rais na jinsi ulivyojieleza ulisema uliteuliwa kuwa mkuu wa wilaya?

**SABAYA:** Ndio

**WAKILI:** Ulikula kiapo cha ukuu wa wilaya?

**SABAYA:** Ndio

**WAKILI:** Kama uliapa unakubaliana na mimi kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria?

**SABAYA:** Upo sahihi

**WAKILI:** Unafahamu kuwa dhima ya umiliki wa laini ya simu ni suala la kisheria?

**SABAYA:** Ndio nafahamu

**WAKILI:** 0758707171 unakumbuka namba hiyo ilizungumziwa hapa mahakamani?

**SABAYA:** Nakumbuka

**WAKILI:** Namba hiyo ilikuwa na usajili wa Lengai Ole Sabaya?

**SABAYA:** Ni sahihi nakumbuka

(Wakili Neema akaiomba mahakama impatie mshtakiwa kidhibiti p3 ambacho ni taarifa zilizowasilishwa mahakamani na kampuni ya mawasiliano ya Vodacom).

**WAKILI:** Picha iliyopo hapo ni ya nani kwenye hiyo karatasi?

**SABAYA:** Ni picha inayofanana na mwonekano wangu

**WAKILI:** Naomba usome maelezo yaliyopo hapo chini

**SABAYA:** Yanaeleza kuwa namba ya simu imesajiliwa na kumilikishwa kwa Lengai Ole Sabaya.

**WAKILI:** Ni kweli kwamba wewe kama Mkuu wa Wilaya ya Hai ulikuwa maarufu, ulikuwa unafahamika na watu wengi?

**SABAYA:** Hapana, mimi sikuwa maarufu

**WAKILI:** Samahani naomba kubadilisha swali. Wewe ulipokuwa Mkuu wa Wilaya mteuliwa wa Rais si ni kweli wananchi wengi walikuwa wanakufahamu

**SABAYA:** Sio kweli

WAKILI: Unaweza kututajia namba ya ufungwa

**SABAYA:** Namba ya ufungwa!

**WAKILI:** Unaweza kutaja sababu zilizopelekea wewe kuwa mfungwa

**SABAYA:** Hiyo sababu bado ipo mahakama za juu inayobishaniwa mimi kuitwa mfungwa.

**WAKILI:** Mheshimiwa naomba kumpa wakili mwingine aendelee.

**WAKILI:** Ni kweli kwamba uteuzi wako ulitenguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**SABAYA:** Sikutenguliwa, nilisimamishwa kazi

**WAKILI:** Ni kweli kwamba ulisimamishwa kazi kwa ajili ya kupisha tuhuma zilizokuwa zinakukabili

**SABAYA:** Sikuwa na tuhuma

**WAKILI:** Kwani barua ya kukusimamisha kazi iliandika umesimamishwa kupisha uchunguzi, ulikuwa uchunguzi wa afya?

**SABAYA:** Barua iliandika kupisha uchunguzi, haikuandika tuhuma zozote. Siwezi kuongelea maelekezo ya Mheshimiwa Rais hapa mahakamani.

**WAKILI:** Unakubaliana na mimi kwamba uchunguzi uliosemwa uchunguzwe ndo matokeo ya kesi iliyokufikisha hapa mahakamani?

**SABAYA:** Sikubaliani maana hakuna uchunguzi uliofanyika.

**WAKILI:** Namba 0758717170 ni kweli kwamba imesajiliwa kwa majina yako?

**SABAYA:** Ndio imesajiliwa kwa jina langu.

WAKILI: Iliwasiliana na 0745978686 siku ya tarehe 22.1.2021, iliwasiliana na mshitakiwa namba mbili?

**SABAYA:** Sijui kwa kuwa hiyo namba sikuwa naitumia mimi.

**WAKILI:** Mroso alisema kuwa tarehe 22.1.2021, mshitakiwa wa pili na wa sita na wa saba walikuwapo kwa Mrombo.

**SABAYA:** Sijui ushahidi wa huyo mtu aliousema

**WAKILI:** Utakubaliana na mimi kuwa mnashtakiwa kwa ushahidi na sio muujiza

**SABAYA:** Sikubaliani na wewe na hakuna ushahidi wowote wa maana ulioletwa kudhibitisha hilo.

**WAKILI:** Ukiwa mtuhumiwa una haki ya kuchagua mahabusu maana ulisema hapa kuwa uliwekwa kwenye mahabusu ya TAKUKURU.

**SABAYA:** Nililalamikia kuwekwa mahabusu siku nane bila kuhojiwa wala kusikilizwa.

**WAKILI:** Ni kweli wewe huna mkopo wowote benki?

**SABAYA:** Ni kweli sina mkopo benki.

# Abiria, madereva, makondakta wahimizwa chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), Kanda ya Kaskazini, kimejitosa kuhamasisha abiria, madereva na makondakta kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19.

Mkurugenzi wa CHAKUA wa kanda hiyo, Solomon Nkiggi, aliliambia gazeti hili jana kuwa, wakati ugonjwa huo unaingia nchini mwaka juzi, walikuwa miongoni mwa wadau waliotoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

"Tumeamua kugeukia uhamasishaji wa chanjo ya corona kwa wadau wetu ambao ni abiria, madereva na makondakta wa mabasi ya mikoani na daladala katika kanda yetu ya Kaskazini," alisema Nkiggi.

Nkiggi alisema, wamejitahidi kuhamasisha wadau wao kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka, kutumia vitakasa mikono na pia kutojazana kwenye basi na sasa wanageukia uhamasishaji wa chanjo.

CHAKUA kwenye kanda yetu tumeweka watu katika stendi zote ambao hufanya kazi hiyo ya kuelimisha umuhimu wa chanjo na kisha kuwaachia wahusika waamue kuchukua hatua sahihi," alisema.

Katibu wa CHAKUA wa kanda hiyo, Godwin Mpinga alisema, serikali ilishatoa mwongozo wa kujikinga na UVIKO-19, na inahimiza chanjo, na kwamba wao wanafikishia wadau wao kile ambacho serikali inataka.

"Chanjo iwe hiari au namna gani, suala la kuchanjwa ni la muhimu, ndiyo maana kila siku tuko kwenye vituo vya mabasi tukihamasisha wadau wetu kuchanja.Tuweke elimu nyingine pembeni, tufuate maelekezo ya wataalamu wa afya kwa ajili ya usalama wa afya zetu," alisema Mpinga.

Alisema makao makuu ya kanda hiyo yapo jijini Arusha ambako kazi ya uhamasishaji wa chanjo ilianzia na kwamba inaendelea kuenea katika vituo vyote vya mabasi vya kanda hiyo.

"Tunashiriki katika kampeni ya chanjo ili kulinda afya za wadau wetu, kwani kila mmoja ana umuhimu wake kwa familia yake, jamii na taifa kwa ujumla, hivyo tunafanya sehemu yetu ya kuhakikisha wanakuwa salama," alisema.

Mpinga alisema,ana uhakika elimu ya kujikinga na ugonjwa huo ambayo imetolewa kwa muda mrefu na CHAKUA katika kanda hiyo, imewafikia wengi, na kwamba hata suala la chanjo wanataka lisambae zaidi.



Madereva wa mabasi yanayofanya safari zake kati ya Iringa na mikoa ya Nyanda za juu kusini; Njombe, Mbeya na Ruvuma, wakiwa katika mgomo mjini Iringa jana, kushinikiza Halmashauri ya Manispaa ya mji huo, kuwaruhusu kuingia stendi ya Ipogolo kushusha na kupakua abiria. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mgomo wa mabasi watikisa Iringa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MADEREVA wa mabasi yanatoa huduma za usafiri katika mikoa ya nyanda za juu kusini; Njombe, Mbeya na Ruvuma, jana waligoma kutoa huduma wakishinikiza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kutengua zuio la mabasi hayo kuingia stendi ndogo ya Ipogolo.

Wakizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mgomo huo, walisema wapo tayari kulipa ushuru wa halmashauri mara mbili kwa maana stendi kuu ya mabasi ya mikoani iliyoko Igumbilo ambako ni mwanzo wa safari na watakapoingia stendi ya Ipogolo kushusha ama kupakia abiria pia watalipa ushuru.

Walisema sababu kubwa inayotajwa na uongozi wa halmashauri ya kutoruhusu matumizi ya stendi hiyo ya Ipogolo ni kukwepa kuua stendi ya Igumbilo ambayo serikali imetumia gharama kubwa katika ujenzi wake, jambo ambalo wao wako tayari kuifanya stendi hiyo kuendelea kuingiza kipato cha halmashauri kwa kulipa ushuru kama kawaida.

Obadia Sanga alisema hadi sasa wao wamekuwa wakitumia stendi ya Igumbilo ambayo ni stendi ya Mkoa wa Iringa, lakini daladala za Mafinga zimekuwa zikitumia stendi ya Igumbilo na stendi ya Ipogolo, jambo ambalo kwao limekuwa likiwatesa kwa kuwa abiria wao wamekuwa wakichukuliwa na daladala za Mafinga na kwenda kuwafaulisha Mafinga kwa pesa ambayo ni ndogo.

"Tunachoomba uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kuturuhusu tutumie stendi ya Ipogolo kushusha abiria tunapotoka Mbeya ama Njombe na tunapokwenda mikoa hiyo tukitokea Igumbilo basi turuhusiwe kuingia Ipogolo kuchukua abiria wa mikoa ya nyanda za juu kusini," alisema

Baadhi ya abiria waliokuwa wakitegemea usafiri huo kwenda mikoa ya nyanda za juu kusini, waliomba uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na madereva kumaliza tofauti yao kwa kuwa wao ndio wanaoteseka kutokana na mgomo huo. Anna Samson alisema kuwa alifika stendi ya Igumbilo jana majira ya saa 11 alfajiri kusafiri kwenda mkoani Mbeya alikokuwa anawahi mazishi, lakini hadi saa tano asubuhi hakuweza kusafiri na kulazimika kusubiri mabasi ya Dodoma ama kutoka Dar es Salaam.

Nipashe ilishuhudia baadhi ya madereva wakilazimika kuendesha mabasi yao bila kupakia abiria kutoka stendi ya Igumbilo zaidi ya kilomita tano hadi stendi ya Ipogolo kuegesha kando kando ya barabara kuu ya Iringa - Mbeya.

Jeshi la Polisi liliwazuia kuendelea kuegesha mabasi yao barabarani ili kulinda usalama wao na watumiaji wengine wa barabara.

Mgomo wa madereva hao ni mwendelezo wa mgomo ulioanza wiki mbili zilizopita ambapo Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, alisema watakutana na madereva na wamiliki hao ili kusikiliza kero yao na kuangalia namna ya kuifanyia kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, akizungumza kwa njia ya simu kuhusiana na mgomo huo, alisema stendi inayotambuliwa ni ya Igumbilo na sio stendi ya Ipogolo, hivyo mabasi yote ynayofanya safari zake nje ya Mkoa wa Iringa yanapaswa kutumia stendi ya Igumbilo na si Ipogolo.

# Mikoa kinara kwa ukeketaji yatajwa

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ametaja mikoa mitano inayoongoza kwa ukeketaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ndani ya viwanja vya Bunge juu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukeketaji wa Wanawake na Watoto itakayofanyika Februari 6, Dk. Gwajima alisema Tanzania inaungana na mataifa mengine duniani kukabili matukio hayo.

Aliitaja mikoa inayoongoza na asilimia kwenye mabano kuwa ni Manyara (58), Dodoma (47), Arusha (41), Mara (32) na Singida (31).

Alisema maadhimisho hayo yatafanyika kwenye mikoa inayoongoza kwa ukeketaji na kitaifa wataungana na mkoa wa Mara pamoja na kongamano la kujadili mkakati wa kukabili ukatili litakuwa Februari 7, mwaka huu.

"Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti wa Afya na Demografia ya Watu Tanzania (TDHS 2015/16), mmoja kati ya wanawake 10 wenye umri kati ya 15 - 49 wamekeketwa. Pia asilimia 35 ya wanawake hao walikeketwa kabla ya kufikisha mwaka mmoja," alisema.

"Kulingana na taarifa hizi, hali ya ukeketaji imekuwa inapungua kutoka asilimia 18 mwaka 1996 kufikia 15 mwaka 2010 na asilimia 10 mwaka 2015/2016," aliongeza.

Kwa mujibu wa Waziri Gwajima, kichocheo kikuu cha vitendo vya ukeketaji ni mila na desturi za baadhi ya makabila katika jamii na kwamba unachukuliwa kama tendo la kumvusha rika mtoto wa kike kutoka utoto na kuwa mwanamke kamili, mzuri na jasiri.

Alisema jamii inayokeketa huamini kuwa msichana aliyefanyiwa hivyo anakuwa tayari kuolewa bila kujali umri wake na kwamba mtazamo huu umesababisha kuongezeka kwa mimba na ndoa za utotoni pamoja na madhara mengine ya kiafya na kisaikolojia.

"Mila hutumika kufanya matambiko na kutii masharti ya mizimu ya baadhi ya jamii zinazoamini kuwa ukeketaji unaondoa mikosi katika familia. Kadhalika, ziko sababu za kiuchumi ambapo ngariba na wazee wa mila hulipwa fedha au mali kadhaa ili kutimiza azma hiyo.

"Kwa upande mwingine, wazazi wa watoto wanaokeketwa huwa na matarajio ya kuwaoza mabinti zao kwa lengo la kupata kipato kupitia mahari na zawadi nyingine zinazotolewa, jamii inaamini kuwa waliokeketwa wanaheshimika nani ya familia zao na katika jamii kwa ujumla. Wengine ni tiba ya ugonjwa wa 'lawalawa' ambao kitaalamu ni Urinary Tract Infection (UTI) ambao ni maambukizi kwenye via vya nje vya uzazi kwa mtoto wa kike au mwanamke," alisema.

Waziri Gwajima alisema ukeketaji una madhara makubwa kwa wanawake na watoto wa kike ikiwa ni pamoja na athari za kisaikolojia kama msongo wa mawazo kwa kuwa vitendo hivyo hufanywa bila ridhaa ya wahusika.

"Madhara ya kiafya kama maumivu makali, kutokwa damu nyingi, kuuguza kidonda, changamoto za kujifungua na uwezekano wa kupoteza maisha, maambukizi ya magonjwa ya ngono, pamoja na maambukizi ya kujirudia kwenye njia ya uzazi na njia ya mkojo (UTI).

Madhara mengine ni virusi vya UKIMWI, mimba kinzani zinazosababishwa na kovu la ukeketaji unaweza kusababisha tundu kati ya njia ya uzazi na uke au njia ya haja kubwa na uke (fistula) hali ambayo inamwathiri mwanamke kwa kiasi kikubwa," alisema.

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## KUANZA KUTUMIKA KWA MFUMO ULIOBORESHWA WA UWASILISHAJI WA RITANI ZA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT)

*Dar es salaam, Alhamis, Februari 03, 2022*

**1.0 Utangulizi**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwatangazia Walipakodi wote waliosajiliwa kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani na Umma kwa ujumla, kuwa imeboresha mfumo wake wa uwasilishaji wa ritani za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Maboresho haya yanalenga kumrahisishia Mlipakodi katika uwasilishaji wa ritani pamoja na ukokotoaji wa Kodi stahiki.

Mfumo ulioboreshwa wa kuwasilisha ritani utaanza kutumika rasmi kuanzia **tarehe 1 Machi 2022** na utatumika katika uwasilishaji wa **ritani za mwezi Machi** ambazo zinatakiwa kuwasilishwa mnamo au kabla ya tarehe **20 Aprili 2022**.

**2.0 Faida Zitokanazo na Mfumo Ulioboreshwa**

Mfumo ulioboreshwa wa kuwasilisha ritani za VAT una faida nyingi kwa watumiaji ikiwa ni pamoja na:-

- Urahisi kwa Mtumiaji ambapo Mlipakodi atahitajika kutumia akaunti moja ya uwasilishaji wa ritani, tofauti na awali ambapo ilimlazimu Mlipakodi kutumia akaunti tofauti kulingana na aina ya ritani ya kodi;
- Ujazaji wa ritani umerahisishwa ambapo taarifa za manunuzi katika ritani ya VAT zitaiingizwa kwa kutumia Namba ya Uthibitisho (Verification Code) tu iliyopo katika risiti ya kielektroniki tofauti na awali ambapo ilimlazimu Mlipakodi kujaza taarifa kadhaa kama Jina la Muuzaji, Namba ya usajili wa VAT, Namba na tarehe ya risiti/Ankara, Kiasi cha manunuzi na VAT katika manunuzi husika;
- Mfumo utawezesha kufanyika kwa marekebisho ya kodi pale yanapotokea kama yalivyoanishwa katika Sheria ya Kodi la Ongezeko la Thamani Sura ya 148 tofauti na utaratibu wa sasa ambapo Mlipakodi alihitajika kuandika barua ya kutoa taarifa kwa Kamishna;
- Mfumo utakokotoa kodi stahiki ya manunuzi wenyewe pale ambapo Mlipakodi atakuwa anajihusisha na bidhaa zinazostahili kulipiwa VAT na zile zilizosamehewa kodi (Partial Exempt Trader); na,
- Mfumo utatoa mrejesho wa upokeaji wa ritani pamoja na makadirio ya kodi mara tu baada ya Mlipakodi kuwasilisha ritani.

**3.0 Namna Mfumo Unavyofanya Kazi na Mambo Muhimu ya Kuzingatiwa**

Mfumo umeboreshwa ili kuweza kuleta ufanisi katika uwasilishaji wa ritani na hivyo kuongeza ulipaji kodi kwa hiari kwa watumiaji. Vitu muhimu vilivyozingatiwa ni pamoja na;

- Mfumo utapatikana katika tovuti ya TRA (www.tra.go.tz) kwa kutumia akaunti ya uwasilishaji wa ritani iliyosajiliwa kuwasilisha ritani za kodi nyingine kama PAYE, SDL, SETPI na ROI;
- **Mfumo utatambua risiti/ankara za EFD zenye namba ya uthibitisho (verification code) tu kwa madai ya kodi ya ongezeko la thamani katika manunuzi. Hivyo, risiti/ankara zote ambazo hazitakuwa na namba ya uthibitisho hazitatambuliwa na mfumo kuanzia ritani za mwezi Machi mwaka 2022;**
- Mfumo utatambua risiti/ankara zenye TIN ya mnunuzi katika madai ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye manunuzi. Hivyo, risiti/ankara zote ambazo hazitakuwa na TIN ya mnunuzi hazitatambuliwa na mfumo kuanzia ritani za mwezi Machi mwaka 2022;
- Mfumo utatambua tu madai ya kodi yatokanayo na malipo ya Ushuru wa Forodha yenye kadhia (TANSAD) halali ya forodha;
- Mfumo utahakiki uhalali wa risiti/ankara na kadhia (TANSAD) ya forodha; na
- Mfumo hautoruhusu kupeleka mbele madai ya kodi ya manunuzi (repayment amount) ambayo yalikuwepo katika mfumo wa awali bali yatatakiwa kuingizwa na TRA baada ya kuhakikiwa.

Ili kuendana na matakwa ya mfumo ulioboreshwa na kuepukana na usumbufu usiokuwa wa lazima, Walipakodi waliosajiliwa na Kodi ya Ongezeko la Thamani wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

- Walipakodi wote wenye madai ya kodi ya manunuzi (repayment amount) kwenye ritani ya mwezi Februari 2022 watatakiwa kuomba marejesho ya kodi (kwa wale wanaostahili) au kutaarifu ofisi ya TRA husika kuhusu kiasi cha madai ya kodi ya manunuzi (repayment amount) kwa ajili ukaguzi/uhakiki kabla ya kuingizwa kwenye mfumo ulioboreshwa;
- Walipakodi wote wahakikishe wanatumia mashine za EFD za Itifaki 2.1 (Protocol 2.1) ili kutoa risiti/ankara zenye namba ya uthibitisho (verification code).
- Walipakodi waepuke kutumia risiti/ankara au kadhia (TANSAD) ambazo sio halali ili kuepuka hatua za kisheria na usumbufu wakati na baada ya kuwasilisha ritani katika mfumo ulioboreshwa; na
- Mlipakodi atatakiwa kutumia namba ya malipo (Tax Debit Number) iliyopo katika hati ya makadirio (tax assessment) ya kodi iliyotolewa ili kufanya malipo ya kodi husika.

TRA itaendelea kutoa miongozo na mafunzo kwa walipakodi na wadau wengine ili kuwaongezea na kuwajengea uelewa wa kutumia mfumo kwa ufanisi. Aidha, TRA inawasihi walipakodi na wadau wengine kuzingatia na kufuatilia miongozo mbalimbali inayotolewa pamoja na kuhudhuria mafunzo mbalimbali yatakayotolewa kuhusu mfumo huu ulioboreshwa.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo Karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

**Tovuti : www.tra.go.tz**
**Namba za Simu bila malipo : 0800 750 075 au 0800 780 078**
**WhatsApp : 0744 23 33 33**
**Barua pepe : huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**A. J. Kidata**
**Kamishna Mkuu**

166904

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mahakama zetu zikatae kuwa sehemu ya rushwa

**UTAFITI** mbalimbali ambao umekuwa ukifanyika na mashirika kadhaa nchini kuhusiana na masuala ya utawala bora, umekuwa ukitaja mahakama kuwa moja ya maeneo ambayo kuna vitendo vya rushwa.

Mbali na utafiti kubainisha hivyo, pia taarifa ambazo hutolewa mara kwa mara na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) zimekuwa zinaitaja mahakama kuwa miongoni mwa ofisi za umma kulalamikiwa na wananchi kwamba kuna vitendo vya rushwa.

Mahakama zetu, ukiacha taarifa za utafiti na za TAKUKURU, zinalalamikiwa na baadhi ya wananchi kwamba baadhi ya watendaji wake wanajihusisha na kuomba pamoja na kupokea rushwa, hivyo kuichafua taswira ya mhimili huo wa dola ambao jukumu lake la msingi ni utiaji haki kwa jamii.

Kuwapo kwa taarifa hizo ni jambo la hatari kwa sababu chombo cha kusimamia haki hakiwezi kutoa haki kwa sababu kuna rushwa, hivyo matokeo yake waliokosa haki yao hawawezi kuridhika bali kulalamika na kukata tamaa kwenda huko kwa mara nyingi kudai haki yao.

Malalamiko yanayotolewa kwamba kuna rushwa kwenye mahakama hayapaswi kupuuzwa badala yake uongozi wa mahakama uyapokee na kuyafanyia kazi ili watumishi wanaoharibu sifa na taswira ya mhimili huo kwa jamii waaanikwe na kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma.

Ni jambo ambalo hakika uongozi wa mahakama utapaswa kulishughulikia haraka kwa sababu hata viongozi wakuu wa nchi wanazo taarifa kuhusu kilio cha wananchi kuhusu rushwa mahakamani.

Kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa juzi jijini Dodoma wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria kwamba bado Mahakama inakabiliwa na vitendo vya rushwa, inathibitisha kwamba kuna kilio kikubwa cha umma kuhusu vitendo vya rushwa katika mahakama zetu.

Alisema hali hiyo inawanyima haki wasionacho na kusababisha malalamiko, na kwamba yapo malalamiko mengi kwa wananchi ya kucheleweshewa haki hususan kwenye masuala ya mirathi kwa wajane na migogoro ya ardhi.

Alisema rushwa bado ipo katika ngazi ya mahakama na kusababisha mwenye haki kukosa haki na asiye na haki kupewa na kuwa pesa zinatembea ingawa sio katika ngazi za juu, lakini katika ngazi za chini bado pesa zinatembea hivyo kusababisha mwenye haki anyimwe haki.

Kwa mujibu wa Rais Samia, Mahakama imepewa jukumu kisheria la kutoa haki na katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo, aliwataka watendaji wa Mahakama watoe haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi na kutazama utu wa mtu.

Unapofikia wakati hata mkuu wa nchi kuwa na taarifa hizo, maana yake ni kuwa wananchi wanalalamikia rushwa kuwakwaza katika kutafuta haki kwenye mahakama zetu, hivyo ni wakati mwafaka kwa wenye dhamana kuchukua hatua.


Tunaona kuwa Jaji Mkuu na viongozi wengine wa mhimili huo kuingilia kati kuchukua hatua kupitia Tume ya Utumishi ya Mahakama ya Tanzania kuwachukulia hatua wahusika ili kukomesha vitendo hivyo.

Inawezekana vitendo vya rushwa havifanyiki katika mahakama zote, lakini kwa kuwa mahakama ni mhimili mmoja, bado unawajibika, hivyo suluhisho ni kuwasaka wahusika na ikiwezekana iwaondoe katika utumishi bila kujali nafasi zao kwa maslahi mapana ya taifa.

Itakumbukwa kwamba rushwa ni moja ya vikwazo kwa maendeleo na ustawi wa jamii, hivyo katika kukabiliana nayo, mahakama ambayo ni chombo cha utiaji haki ijisafishe kwanza kabla ya kutoa hukumu za kuwapa haki wanaolalamika na kulalamikiwa kortini.

Ni matarajio yetu kwamba kauli ya Rais Samia ni angalizo kwa watoa haki kujitathmini uadilifu na weledi wao katika kutekeleza majukumu yao katika kuihudumia jamii pamoja na mhimili huo kuchukua hatua dhidi ya wala rushwa kwa lengo la kujisafiisha kwa umma ili uaminike.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kampuni za simu tafakarini adha hii kutuungisha mitandao 'ujanjaujanja'

Na Anthony Gervas,

**KURUNZI** langu la wiki hii linaangazia uwepo wa kero kubwa inayowaumiza wateja au watumiaji wa muda wa maongezi kwenye simu, wanapojiunga vifurushi vya wiki au mwezi kutoka katika baadhi ya mitandao ya kampuni za simu nchini.

Kero hiyo imekuwa ya kudumu kwa wateja ambao pengine maisha yao ni ya chini, kwamba wakiweka pesa za kujiunga katika vifurushi kwenye mitandao ya simu wanayotumia, lakini wanajikuta risiti ya mtiririko wa kujiunga inafichwa mara baada ya kuweka vocha.

Mfano mteja anaweka shilingi 1,000 au 2,000 kujiunga kifurushi cha wiki, ambacho ameonyeshwa kwenye mtiririko wa mtandao kabla hajaweka pesa pamoja na dakika za kujiunga,lakini cha ajabu akiweka tu pesa risiti hiyo inapotea na kuletewa nyingine kujiunga ambayo ni dakika za saa 24,badala ya wiki.

Pengine ameweka fedha shilingi 5,000 kujiunga kifurushi cha wiki au mwezi, baada ya kuweka pesa hiyo ili ajiunge mtiririko uliokuwepo unaondolewa na kubadilishiwa aidha ajiunge masaa 24 au aongeze pesa shilingi 10,000 ndipo ajiunge dakika za mwezi, je huo ni uungwana kweli kwa watoa huduma hao wa simu ?

Zipo kampuni nakiri hazifanyi udanganyifu huo, lakini baadhi yake zimeona ndiyo biashara nzuri kuwaumiza wateja au watumiaji, hawajui kwamba hiyo ni kero kwa wananchi wenye hali za chini.

Niulize, kwanini mnafanya tabia hizo za kuwavuruga wateja wenu, pengine wengine wanalazimika kuchukia na kuhama mtandao wa kampuni ile na kusajili laini ya kampuni nyingine?

Nawauliza ninyi baadhi yenu wenye kampuni za mitandao ya simu mnaofanya hivyo, mnatupa kero sisi wateja wenu, tabia hizo zinatoka wapi, kwanza mnajichafua wenyewe dhidi ya dhamana na uaminifu wa kuheshimika, pia wateja wanafikia hatua ya kuuchukia mtandao a kuhamia kwingine.

Hebu fikiria unakuta mtu amejinyima kununua hata unga au kutumia pesa hizo kwenye huduma zingine, akaweka vocha ajiunge ili aweze kuwasiliana na mtu apate huduma nyingine, halafu kampuni tena inamuongezea shida na mawazo mengine,hiyo ni kero kubwa kwetu wateja.

Tukiachana na hilo, unakuta mteja ameweka salio lake kwenye simu,mara pesa zinapotea au anaambiwa anadaiwa alikopa muda wa maongezi bila yeye kujua, hizo tabia wanazotufanyia ni sahihi kweli, hawaoni wanatuudhi watu wengi?

Wahusika wa kampuni hizo, pia wasimamizi kitaifa nasema ukweli ulivyo, acheni kuwaudhi wateja wenu kwa kutumia staili hiyo. Sisi kuwa wateja wenu, ina maana tunawapenda.

Dhamana husika kama vile Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) nanyi nawadokezeni vaeni miwani mtusaidie wananchi tunaumizwa, pia kwako waziri mwenye dhamana hii ni huduma muhimu kwetu.

Binafsi, mimi ni shuhuda ninayeona kwa mbali hayo, miongoni mwa wateja wenzangu, huwa wanakereka na kulalamika sana juu ya hayo ninayolalamikia.

Watanzania wenzangu, sasa tuungane pamoja kukemea adha hii kutoka huduma za simu, daima, tusibaki kimya huku tunaendelea kuumia, bali tupazeni sauti zetu ili waache kututendea dhambi hiyo.

Wapo watu wengi ambao wamekuwa wakilalamika kutokana na tabia hiyo, mwishowe wanaamua kuhamia mitandao mingine ili kuepuka udanganyifu huo, sababu huenda wanaofanya hivyo ni wahusika ndani ya kampuni, bila ya wawekezaji kujua.

Serikali tunaiomba itulinde na sisi watumiaji wa mitandao sababu tunayofanyiwa kupitia adha ya baadhi ya vifurushi mbalimbali vya kujiunga hayapendezi.

Nasisitiza kwamba haki inapaswa kuwapo ikijengewa mazingira ya kudumu,binafsi nikiamini suala la kuhama mitandao kukimbia kero,si suluhu bali njia sahihi ni kuzifuta kero za ndani wateja wafaidi uhuru wao wa mawasiliano.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka (kulia), akitoa maagizo kwa mgodi wa Katavi Mingi Company Limited wa Mkoa wa Katavi kuzingatia utunzaji wa mazingira wakati wa shughuli za uchimbaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatoa neno matukio ya mauaji

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imezitaka kamati za kupinga ukatili kwenye maeneo mbalimbali nchini, kutekeleza majukumu yake ipasavyo na jamii kushiriki kukabili matukio hayo yaliyoshika kasi.

Aidha, imesema inafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa mwaka 2017/18 na 2021/22 wa kupambana na mauaji na ukatili kwenye jamii.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, alipokuwa akimjibu Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavango, aliyetaka kujua moja ya changamoto anayoanza nayo (Waziri) kwenye wizara hiyo ya mauaji yanayoendelea kwenye jamii yanayotokana na jinsia ikiwamo mume kuua mke, mke kuua mume na mtoto kuua mzazi kwa sababu ya mali.

Gwajina alisema: "Tunao mkakati wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto, Mpango wa taifa uliozinduliwa mwaka 2017/18 unakwenda mpaka 2021/22."

"Umeandaa kamati kwenye vijiji vinavyoongozwa na wenyeviti wa serikali za vijiji, mtaa, kata, halmashauri mpaka taifa na mkoa ukiwamo," alisema na kuongeza."

"Kamati hizi tumeshazipelekea maelekezo na leo tunaenda kuadhimisha siku ya kupinga ukeketaji Februari 6. Hii ni fursa ya kuziamsha hizi kamati zifanye kazi yake."

Waziri alisema iwapo kamati hizo zitatekeleza majukumu yake yaliyomo kwenye mwongozo itaweza kudhibiti ukatili unaotokea kwenye jamii kwa kuona viashiria husika na kuvitolea taarifa kwenye vyombo vya dola.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku ya kimataifa ya kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto, Dk. Gwajima alisema kamati hizo zinajumuisha viongozi wa dini ambao watatoa huduma za kiroho, asasi za kiraia, viongozi maarufu kwenye jamii na wawakilishi wa makundi mbalimbali.

"Silaha za kupinga ukatili zipo ndani ya mikono yetu wanajamii, tushirikiane ipasavyo nasi tunazifuatilia hizi kamati zifanye kazi yake inavyotakiwa ili kuzuia matukio ya ukatili,"

# Maisha ya Mwalimu Nyerere kuwa urithi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau imezindua mpango wa miaka 10 wa kuenzi na kusherehekea urithi wa maisha ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Mpango huo unalenga kuwashirikisha wadau ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu mchango wa Mwalimu Nyerere kitaifa na kimataifa.

Pia umuhimu wa kuandaa, kutangaza, kumuenzi, kukusanya, kuendeleza, kuhifadhi na kutangaza rasilimali za urithi wa Mwalimu Nyerere kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho ili kukuza na kuendeleza utalii.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mpango huo wa miaka 10 wa maadhimisho ya Mwalimu Nyerere unaokwenda kwa jina la 'Mwalimu Nyerere @100'.

"Maadhimisho ya miaka 100 ya Mwalimu Nyerere (Mwl.Nyerere @100) kama sehemu ya kutekeleza mpango wa miaka 10 wa kuenzi na kusherehekea urithi wa maisha ya mwalimu Nyerere yanatarajiwa kufika kilele tarehe 13 Aprili 2022, Butiama mkoani Mara tarehe ambayo ndiyo kama angekuwa hai angetimiza miaka 100," alisema Dk. Ndumbaro.

Aidha, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuenzi na kusherehekea mchango maridhawa wa Mwalimu Nyerere katika nyanja mbalimbali kitaifa na kimataifa.

"Mwalimu Nyerere katika kipindi chake cha maisha yake amefanya mambo mengi sana ambayo sisi kama wizara tunaweza kuyatumia kama urithi wetu kwa kuyatangaza ili yaweze kufahamika na watu wengi. "Mwalimu Nyerere alikuwa maarufu sana nchi za nje kuliko hata hapa kwetu, hivyo kupitia mambo aliyofanya tutakwenda hadi nje ya mipaka yetu kuyatangaza ili vizazi vya nje kuyajua mambo kama ukombozi wa mataifa ya Afrika," alisema Dk. Ndumbaro.

Kadhalika, alisema katika mpango huo watahakikisha kila jambo alilolifanya Mwalimu Nyerere wanalitumia katika kutangaza urithi aliouacha katika maisha yake toka anazaliwa.

"Kuna sehemu Songea tuliambiwa kuna mti aliutumia kuhutubia wananchi wakati wa kutafuta uhuru wa Taifa letu hadi leo bado upo, lakini kuna baiskeli aliitumia vyote, hivyo tutahakikisha kuwa tunavikusanya na kuviweka sehemu moja ambayo itatumika kama makumbusho ya taifa," alisisitiza. Waziri alisema kuelekea kilele hicho matukio mbalimbali yanatarajiwa kufanyika ikiwamo mikutano ya wadau, mashindano ya baiskeli, matembezi ya hiyari na ngoma za asili.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Francis Michael, alisema mpango huo umeainisha kazi ambazo zitatekelezwa na taasisi mbalimbali ambapo wizara yake ndiyo itaratibu shughuli zote.

# BoT yaridhishwa na mwenendo uchumi

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imepitia utekelezaji wa sera ya fedha na mwenendo wa uchumi wa ndani na wa dunia na kuridhishwa na utekelezaji wa sera ya fedha na mwenendo mzima wa uchumi.

Pia, imeidhinisha benki kuendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi, ili kusaidia kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwenye vyombo vya habari na BoT, Msimamo huo umechukuliwa kwa kuzingatia matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia tatu hadi tano.

Kwa mujibu wa BoT, Kamati hiyo imeridhishwa na ukuaji wa uchumi wa Tanzania Bara, uliokua kwa wastani wa asilimia 4.9 katika robo tatu za kwanza za mwaka 2021.

"Ukuaji huu umechangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, uchimbaji madini, viwanda na usafirishaji. Aidha, Kamati ilibaini ongezeko la mfumuko wa bei kufikia asilimia 4.2 Desemba mwaka jana kutoka asilimia 3.8 Julai mwaka huo zilizotokana na changamoto za ugavi, hata hivyo mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia tatu hadi tano."

Pia, ilisema uchumi wa Zanzibar umekua kwa kasi ya kuridhisha kufikia asilimia 8.8 katika robo ya tatu ya mwaka jana ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, hususani utalii.

"Mfumuko wa bei uliongezeka kidogo, ukichangiwa na bei zisizo za vyakula, hata hivyo umeendelea kubaki ndani ya lengo la chini ya asilimia tano."

Ilisema imeridhishwa na kuimarika kwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kufikia asilimia 7.8 na asilimia 10 Novemba na Desemba mwaka jana, kutoka chini ya asilimia tano kwa sehemu kubwa ya mwaka jana.

"Mwenendo huu ni sambamba na lengo la ukuaji wa asilimia 10.6 kwa mwaka 2021/22 na ulichangiwa na utekelezaji wa sera ya fedha yenye kuongeza ukwasi katika uchumi, utekelezaji wa hatua za ziada za kisera zinazolenga kuchochea utoaji wa mikopo na kushusha viwango vya riba pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kufuatia kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia."

Sekta ya nje imeendelea kuimarika kutoka kwenye athari za janga la UVIKO-19, ikidhihirishwa na kurejea kwa shughuli za utalii.

Ilieleza kuwa akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 6.4, kiasi kinachotosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa miezi 6.6 na kwamba utekelezaji wa bajeti ya serikali uliendana na matarajio kutokana na kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato na misaada na mikopo kutoka nje.

"Kamati imeridhishwa na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa ndani pamoja na wa dunia, na hivyo matarajio ni kuwa malengo ya sera ya fedha yaliyowekwa katika Tamko la Sera ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 yatafikiwa."

# Mchimbaji madini asakwa tuhuma vifo watu watatu

**Na Mohab Dominick,**
NYANG'WALE

JESHI la Polisi mkoani Geita linamtafuta Chacha Dunde kwa tuhuma za kusababisha vifo vya watu watatu waliofukiwa na kifusi cha udongo katika Mgodi wa Igalula wilayani Nyang'hwale mkoani Geita.

Ofisa Madini Mkoa wa Kimadini Mbogwe, Joseph Kumburu, alidai Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, Jamhuri Wiliam, amelielekeza Jeshi la Polisi limsake na kumkamata mtuhumiwa huyo na kumfungulia mashtaka ya mauaji.

"Mkuu wa wilaya amekwishatoa maelekezo huyo mtuhumiwa atafutwe na afunguliwe kesi ya mauaji, lakini sisi kwa upande wa madini mtu huyo haruhusiwi kufanya shughuli zozote za kimadini kwenye mkoa huu na mkoa mwingine wa kimadini na tutafuatilia kama kuna mchimbaji anashirikiana naye tunaanza naye," alisema Kumburu.

Alidai kuwa mtuhumiwa huyo alilazimisha watu hao waingie kwenye machimbo ambayo serikali ilikwishatoa maelekezo ya ukarabati kutokana na ubovu wake, lakini hakuzingatia, hivyo kusababisha vifo hivyo.

Alidai kuwa kwenye eneo hilo bado kuna 'maduara' matano ambayo idara ya ukaguzi ya mgodi wa Igalula ilielekezwa kukagua na kuyafanyia ukarabati.

Alifafanua kuwa 'duara' moja la Peter James ambaye kwenye ukaguzi alikimbia, halikufanyiwa ukaguzi lakini alirudi na kutaka kuendelea kuchimba dhahabu wakati mradi wake unahatarisha usalama wa maisha ya watu.

"Na kwa taarifa iliyoko Peter anatishia watu, agizo langu kama ofisa madini, huyo mtu haruhusiwi kukanyaga hapa na migodi mingine mpaka akaripoti polisi kwa maelekezo ya mkuu wa wilaya, na mmiliki wa duara namba 4E naye haruhusiwi kukanyaga hapa vinginevyo aje na barua ya ofisi ya madini kwenye eneo hili, akiwamo Kulwa Luchonga wa duara namba 239 B naye haruhusiwi," Kumburu alielekeza.

Alimtaja mwingine ni Abubakari mwenye duara namba 7B ambaye haruhusiwi kufika mgodini bila kibali cha ofisi ya madini na kuagiza maduara yao yote ambayo yanatuhuma yazuiliwe kwa muda mpaka hapo serikali itakapojiridhisha ikiwa ni njia mojawapo ya kukinga watu wasiingie maduarani kwa lengo la kuiba mali.

Msimamizi wa mgodi wa Igalula, Godfey Mbasa, alidai kuwa baada ya kuzuia shughuli kwenye machimbo husika, mpaka zitakapoimarishwa kutokana na ubovu, Chacha amekuwa akimtishia maisha na kwa kumdhuru kwa namna yoyote ile.

"Duara lililosababisha ajali ni lile lililozuia ofisa madini na hata wataalamu wengine katika ofisi yako nao walizuia, lakini mwenye duara kwa ukorofi mpaka sasa hata mimi ninayekupa taarifa hizi huyo bwana ananitishia, hivyo maisha yangu yapo hatarini," alilalamika.

Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, William, alisema serikali haitavumilia kuendelea kushuhudia ajali za mara kwa mara katika mgodi huo, akiwataka wachimbaji kuwa makini na kuchukua tahadhari haraka pindi wanapobaini kutozingatia kwa usalama wao.

Katika tukio hilo waliofariki dunia ni Yohana Issa, mkazi wa Kabindi, Biharamulo; Bahati Mlongo, mkazi wa Kilombolo, Lwamgasa; na Sheria Juma, mkazi wa Ngemo, Mbogwe.



Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James (wa tatu kulia), Meneja Mwandamizi wa Uwekezaji kwa Jamii wa Benki ya CRDB, Joyceline Makule (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari Mashujaa, Prof. Alphonce Kyessi, wakikata utepe kufungua rasmi madarasa mawili katika shule hiyo, eneo la Sinza 'B', Dar es Salaam jana, yaliyojengwa kwa udhamini wa benki hiyo na madawati 125 vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 50. Wengine ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubungo, Dk. Peter Nsanya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANAPA yatia saini bil. 15/- utalii kusini

**Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limeingia makubaliano ya ununuzi wa magari na mitambo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 15 kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika hifadhi za taifa.

Makubaliano hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) unaoendeshwa chini ya mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Hifadhi zitakazonufaika katika makubaliano hayo ni Ruaha, Mikumi, Udzungwa na Nyerere.

Utiaji saini wa makubaliano hayo ulifanyika jana makao makuu ya TANAPA jijini hapa ambapo Kamishna wa Uhifadhi, William Mwakilema alitia saini mikataba na kampuni za Al Mansour Auto EA Tanzania Ltd na Hughes Agricultural Tanzania Ltd, zilizoshinda zabuni ya kusambaza magari na mitambo hiyo.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini mikataba hiyo, Kamishna Mwakilema alizitaka kampuni hizo kukamilisha taratibu zote kwa haraka kwa mujibu wa mikataba yao, ili kuwezesha upatikanaji wa mitambo na magari hayo kwa wakati.

Kamishna Mwakilema alishukuru serikali kwa juhudi za kuhakikisha miundombinu ya utalii nchini inaimarika na hivyo kuwawezesha watalii wengi kufika kwa urahisi katika vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Pia aliishukuru Benki ya Dunia kwa kufadhili mradi huo wenye lengo la kuendeleza shughuli za utalii katika hifadhi za kusini.

"Upatikanaji wa vifaa hivi utapelekea hifadhi hizi kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuendeleza hughuli za hifadhi pamoja na kuimarisha miundombinu ya utalii na hatimaye kutimiza lengo la serikali la hifadhi zote kuchangia uchumi wa nchi yetu kupitia Utalii," alisema.

Awali, akitoa taarifa ya makubaliano hayo, Mratibu wa Mradi wa REGROW kutoka TANAPA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Betrita Lyimo, alitaja idadi ya magari na mitambo 44 itakayonunuliwa kuwa ni pamoja na Water Bowser tano, Fuel Bowser mbili, Tipper dump truck 17, Concrete mixer tano, Low loader trailer mbili, Expedition truck tatu, Mobile workshop tano, Cinema van nne, na Minibus moja.

Mitambo mingine ni Trekta (7), Mower machine za Trekta (6), Water bowser za trekta (8) na trela za trekta (tani 5 ) tisa.

Maeneo makubwa yatakayoshughulikiwa ni ukarabati wa barabara zipatazo kilomita 2050 hifadhini, kujenga majengo ya watumishi pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja 14 vya ndege vilivyoko kwenye maeneo husika pamoja na matengenezo ya mitambo na magari.

# RC Katavi alalamikia wavamizi misitu

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa**
KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amelalamikia uvamizi wa wananchi kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na kusababisha uharibifu wa mazingira kwenye misitu mbalimbali.

Alitoa malalamiko hayo wakati wa ziara ya Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, na ujumbe wake.

Ujumbe wa NEMC ulienda mkoani humo kutembelea mgodi wa Katavi Mining Company Limited kwa ajili ya kuangalia kama utunzaji wa mazingira unazingatiwa wakati shughuli za uchimbaji madini zikiendelea.

RC alisema kuna wananchi wanatoka kwenye mikoa mbalimbali na wengine wa ndani ya mkoa ambao wamekuwa wakiingia na kufanya shughuli za kibinadamu kama kukata miti kwa ajili ya kupata mashamba na kuingiza mifugo kwa ajili ya kutafuta nyasi nzuri na maji.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni wananchi wengine kuingia kwenye hifadhi za mkoa huo kwa ajili ya kufanya ujangili wa wanyama mbalimbali walio kwenye hifadhi hizo.

Alisema wananchi hao wamekuwa wakivamia kwenye maziwa na mabwawa ambako wamekuwa wakifanya uvuvi haramu na kuharibu mazingira.

"Tunapata changamoto kubwa ya watu kuhamia kutoka mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita, Mwanza na Tabora kwa sababu kuna wimbi kubwa la wananchi wanatoka kule kuja hapa kutafuta maji, ardhi nzuri yenye utuba na malisho ya mifugo," alisema.

"Kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu raia anaruhusiwa kuishi popote anapotaka ila tunawataka wazingatie sheria na taratibu za sehemu husika, tunawapenda ila tunachohitaji wafuate sheria wasiharibu mazingira yetu," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa NEMC, Dk. Gwamaka, alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa michache nchini yenye madini adimu. Alisema uwekezaji uliofanywa na mgodi huo ni mkubwa na muhimu kwa uchumi wa nchi kwani wanaweza kuchambua madini ya aina nyingi kwenye mwamba mmoja.

Alisema kwenye wilaya zote mi-amba ipo mingi lakini wachimbaji wa dhahabu wamekuwa wakiacha madini mengine lakini mgodi wa Katavi umeweka mtambo wa kuchambua madini mengi kutoka kwenye mwamba.

"Kimazingira wote tunafahamu wachimbaji wadogo wanatumia zebaki kupata madini na wakimaliza kazi zao ile zebaki inabaki sasa ni uchafuzi wa mazingira ila mgodi wa Katavi wanachukua mabaki kutoka kwa wachimbaji wadogo wanayachuja na zebaki inabaki sehemu moja tunaokoa mazingira yetu," alisema.

## Mzee wa TASAF alivyotatua kero ya maji Kabuku

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa** HANDENI

MZEE wa miaka 81, Suzan Mhando, mnufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini, unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), amegeuka kuwa mkombozi kwa wananchi wa Kabuku wilayani Handeni mkoani Tanga, baada ya kutatua tatizo la maji ambalo limekuwapo kwa muda mrefu katika eneo hilo.

Baadhi ya wananchi wa soko la Kabuku Kaskazini wakizungumza sokoni hapo, walisema kwa muda mrefu eneo hilo limekuwa likikumbwa na tatizo la maji, lakini kwa sasa kumepatikana ahueni baada ya bibi huyo kutumia pesa anayopatiwa na TASAF kuchimba kisima cha maji ambayo ndiyo yanayotumika kwa wakazi wote wa eneo hilo pamoja na wafanyabiashara sokoni hapo.

Monica Dunstan ni miongoni mwa wafanyabiashara katika sokoni hapo, alisema miaka mingi katika eneo hilo kumekuwa na tatizo la maji licha ya kuwapo na umuhimu wake kulingana na bidhaa zinazouzwa hapo na hivyo kuwalazimu kununua ndoo moja kwa Sh.500 kutoka kwa wale wanaokwenda kununua kwa jumla kutoka sehemu nyingine kunakopatikana huduma hiyo ya maji.

"Kabla ya bibi huyu kuchimba hiki kisima, maji tuliyokuwa tunatumia ni yale ya kununua kwa ndoo Sh. 500 ambayo nayo walanguzi wanayafuata mbali, na hutulazimisha tununue kwa jumla ndoo tano kwa Sh. 25,000 wakisema bila kufanya hivyo hailipi na hawakubali kutuuzia," alisema Monica.

"Na kama huna hiyo pesa ya kununua kwa jumla unakosa maji, na kutokana na umuhimu huwa inatubidi tuungane ndio tuchukue kwa namna hiyo. Lakini tangu huyu bibi achimbe kisima cha maji, kimekuwa ni mkombozi kwa soko hili lote hata kwa wakazi wanaomzunguka. Yeye anatuuzia kwa bei ndogo ya Sh. 100 tu kwa ndoo moja." Neema Ali, alisema mbali na kutumia maji hayo ya kisima kusafishia bidhaa zao sokoni hapo, pia wanayatumia kwa ajili ya matumizi mengine ya nyumbani ikiwamo kupikia na kufulia.

"Tunaishukuru sana TASAF, si tu kwamba imemsaidia huyu bibi Suzan, bali pia imetusaidia na sisi, shida ya maji tuliyokuwa tunaipata awali ilikuwa kubwa sana," alisema Neema.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho cha Kabuku Kaskazini, Kitumbo Waziri, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo la maji katika eneo hilo na kwamba kwa sasa maji ya kisima cha bibi huyo ndiyo yamekuwa mkombozi kwa wananchi wake.

Kwa upande wake bibi huyo, alisema siri ya kufanikiwa kuchimba kisima hicho ni kujiwekea akiba ya pesa kidogo kidogo anayopatiwa na TASAF.

"Tangu niingizwe TASAF nilianza kuweka pesa kidogo kidogo huku nafanya biashara ndogo mpaka nikafikia hatua ya kuchimba hiki kisima," alisema bibi Suzan.

Alisema ndoo moja ya maji huuza Sh. 100 na kwamba kwa siku hukusanya Sh. 15,000 mpaka Sh. 20,000 kutokana na mauzo ya maji hayo.

# Aweso: Wiki ya Maji si kuvaa tisheti na kofia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza maadhimisho ya Wiki ya Maji yatumike kufanya tathmini ya upatikanaji wa huduma ya maji na kuwapima watendaji katika utekelezaji wa miradi ya maji badala ya kusherehekea kwa kuvaa tisheti na kofia.

Aidha, ameagiza mabwawa yote yanayojengwa kwa ajili ya kuvuna maji yazingatie viwango na thamani ya fedha ili kuleta tija kwa wananchi.

Aweso aliyasema hayo juzi kwenye hafla ya utiaji saini wa uchimbaji wa mabwawa kati ya Wizara ya Maji na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Alisema wiki hiyo itumike kuzindua miradi ya maji iliyojengwa na kujifanyia tathmini.

"Tunaenda wiki ya maji tunataka wiki hii sio iwe ya mapambio wala ngonjera, bali twende tukazindue miradi ya maji kila kona nchini na nikuombe Mtendaji Mkuu wa RUWASA wiki hii ya maji na Katibu Mkuu mweleze itumike kufanya tathmini sio tu wiki ya maji tuvae tisheti na kofia tunashangilia tu hapana bali iwe wiki ya matokeo ya uhalisia wa kuanzishwa kwake twendeni tukazindue hiyo miradi wiki nzima," alisema.

Aliongeza "Ifanyike tathmini kama Mhandisi wa Mkoa hana mradi wa kuzindua huyo achana nae, wakati mwingine tunashindwa kufikia hatua na kuleta matokeo kwa sababu watu hawana miradi, inakuwaje wewe unakaa miaka mitano hujawahi hata kuzindua mradi hawa watu tutawatafutia shughuli za kufanya maana ni lazima tujipime, kama kuna mtu anaona hana mradi wa kuzindua bora ajimwagie dumu la maji."

Kuhusu ujenzi wa mabwawa, Aweso alisema hatakubali kuona mvua inayonyesha nchini inapotea bure wala kuharibu miundombinu ilhali wananchi hawana maji na badala yake yatavunwa kupitia mabwawa yatakayojengwa na yaliyoko.

"Tuna takribani mita za ujazo zaidi ya bilioni 126 za maji ardhini ambapo kati ya hizo mita bilioni 105 yapo juu ya ardhi, bilioni 21 yapo chini hivyo haipendezi na wala haifurahishi mvua kwetu inakuwa maafa badala ya fursa," alisema.

Alibainisha kuwa mabwawa hayo yatahifadhi maji ambayo yakatumika hata na sekta nyingine kama kilimo, mifugo.

"Jukumu la wizara ni kutunza vyanzo vya maji na kuhakikisha Watanzania wanapata majisafi na salama," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Mhandisi Clement Kivegalo, alisema kuna tatizo lilijitokeza la vyanzo vya maji vilikauka na kusababisha kufanyika utafiti na kubaini hawakutumia wataalamu wao wa ndani kuvitafuta.

"Tuliona kitu cha kwanza kuingia makubaliano na wenzetu raslimali za maji ili shughuli ya kutafuta chanzo cha maji. Na kuhitimisha kwamba hiki kinafaa na tujenge miundombinu na tukasema hii kazi ifanywe na ofisi za mabonde," alieleza.




Meneja Masoko wa bahati nasibu ya Biko Mshiko Nje Nje, Goodhope Heaven (kushoto), akishiriki kukabidhi Sh. milioni 10 kwa mshindi Karimu Malisawa Mwema (katikati), katika Tawi la Benki ya CRDB Palm Beach, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Balozi wa Biko, Kajala Masanja (wapili kushoto), Meneja wa Tawi hilo, Pendo Kitula (wapili kulia) na Meneja Huduma kwa Wateja, Catherine Momburi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbegu 1,000 maharage, soya kuzalishwa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKALA wa Mbegu Tanzania (ASA), imejipanga kuzalisha tani 1,000 za mbegu ya maharage ya soya na kutumiwa na wakulima katika msimu ujao wa kilimo 2022/23, baada ya kupokea tani 100 za mbegu hizo na kuanza kuzalisha kwenye mashamba yake.

Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, alisema kuwa kutokana na uhaba wa upatikanaji wa mbegu hizo, waliziagiza kutoka Zambia na kuzipanda katika mashamba yao Mkoa wa Arusha.

Alisema mahitaji ya soya sokoni kwa wakulima kwa sasa ni makubwa kutokana na serikali kutafuta na kufungua masoko likiwamo la China.

Naye Mkurugenzi wa Uzalishaji wa ASA, Justin Ringo, aliwataka wakulima wa zao hilo kutembelea kwenye vituo vya mauzo vya ASA kwa ajili ya kupata mbegu za maharage ya soya kwa msimu huu wa kilimo.

Alisema wameingiza tani 100 ambapo tani 30 kati ya hizo watasambaza kwa wakulima na zilizobaki zitapandwa kwenye mashamba ya ASA na chache zitawekwa kwenye vituo kwa ajili ya mauzo.

Alisema ASA imejipanga kuzalisha mbegu hizo katika mashamba yake yaliyoko Dabaga mkoani Iringa kwa kupanda jumla ya hekari 250 na Arusha hekari 250.

Aidha, alisema zao la soya halikuwa likilimwa nchini kwa sababu ya ukosefu wa mbegu na masoko ya uhakika, na kwamba tangu serikali itangaze upatikanaji wa masoko kwa zao hilo ndani na nje ya nchi wakulima wamekuwa wakihitaji katika msimu wa kilimo kwa ajili ya kukuza uchumi wao.

Akipokea mbegu kwa niaba ya wakulima kutoka vijiji vya Wilaya ya Morogoro Katibu Tawala Msaidizi Idara ya Uchumi na uzalishaji mkoani Morogoro, Dk. Rozalia Rwegasira, alisema wakulima hao watapata mbegu kupitia mradi wa kilimo mahiri unaolenga kumfundisha mkulima kutambua mnyororo wa thamani wa mazao ya maharage ya soya.

Alisema lengo hasa ni kuhamasisha kilimo cha zao hilo na kuwafanya wakulima kuona tija katika uzalishaji wa zao hilo.

Naye Mratibu wa mradi huo, Ernest Mkongo, alisema wanaanza na wakulima 100 ambao watafundishwa namna bora ya uzalishaji wa maharage ya soya pamoja na kupatiwa kilo 20 za mbegu ili uzalishaji uwe wa tija, na kwamba baada ya kuona matokeo kwa wakulima hao wataendelea na maeneo mengine.

"Tunatarajia kuwa katika kila hekali moja mkulima azalishe kilo 1,000, wakulima pia watafundishwa namna ya kutengeneza bidhaa pamoja na kupatiwa vifaa na kuongeza thamani ya mazao yao na kuondoa changamoto ya soko," alisema Mkongo.

# Serikali kutoa ruzuku maparachichi

SERIKALI imesema inafuatilia kwa karibu mikoa mitano inayozalisha maparachichi kwa kutumia taasisi za utafiti, huku ikitengeneza kanuni za mbegu ili kuondoa uuzaji holela wa miche ambayo itaua zao hilo.

Hayo yalisemwa jana bungeni na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Shally Raymond, na swali la nyongeza la Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga.

Alisema mwongozo wa mbegu utazinduliwa hivi karibuni na kwamba itaanza programu ya kuzalisha miche na kugawa bei ya ruzuku kwa kuwa kwa sasa wakulima wananunua kati ya Sh. 5,000 na 6,000 kwa mche mmoja.

"Tutajenga maeneo maalumu yatakayokuwa kati ya Iringa na Njombe, Dar es Salaam na Kilimanjaro, ambayo yatatumiwa na wanunuzi wa nje ambao watalipia na kuwa na alama bidhaa zimetoka Tanzania,"alisema.

Katika swali la nyongeza, Sanga alitaka kujua mpango wa serikali kugawa mbegu bure kama ilivyofanya kwenye michikichi, pamba na korosho, kwa kuwa wakulima hawana uwezo na umuhimu wa zao hilo ni dhahabu ya kijani.

Katika swali lake la nyongeza, Raymond alitaka kujua ni lini serikali itatoa ruzuku kwa mazao ya mboga ili yalimwe kibiashara kwa sababu shida kubwa ni upatikanaji wa mbegu.

Pia alitaka kujua mpango wa serikali kuwawezesha wanawake wa mkoa wa Kilimanjaro na taasisi zenye mashamba makubwa, kuwasaidia walime maparachichi kwa wingi. Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, alisema ushauri wa mbegu na ruzuku umepokelewa na kwamba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeendelea kuimarishwa ili kuja na utafiti wa kusaidia kupata mbegu zenye tija.

Kuhusu mashamba yasiyotumika, alisema dhamira ya serikali ni kongeza uzalishaji wa parachini ambao kwa sasa ni tani 48 na lengo ifikapo 2025 zifike tani 140 na kuongeza usafirishaji nje.



Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, akichangia hoja kwenye vikao vya Bunge vinavyoendelea jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wizara kudhibiti miradi chechefu

SERIKALI imesema itafuatilia kwa karibu miradi yote chechefu ndiyo maana imeunda kikosi kazi cha ufuatiliaji ili kuchukua hatua kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma za maji.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Buchosa, Erick Shigongo.

Mbunge huyo alitaka kujua ni lini waziri atatembelea mradi wa Rumeya, Nyakaliro, Kalebezo hadi Nyehunge wenye thamani ya Sh. milioni 1.6 ambao ni kichefuchefu kwa kuwa ulijengwa chini ya kiwango na sasa mabomba yanapasuka wananchi hawapati maji.

"Ni lini serikali itapeleka wataalamu kuchunguza na kugundua waliohusika na ubadhirifu wa mradi huo na kuchukua hatua?" alihoji.

Naibu Waziri Mahundi aliahidi kutembelea mradi huo na kuelekeza wataalamu kwenda kuchunguza mradi huo ili wananchi wapate maji.

Awali, akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalumu, Anatropia Lwehikila, aliyetaka kujua ni lini serikali itawafikishia maji wananchi wa wilaya ya Kyerwa kwa kutengeneza miundombinu ya kupeleka maji kwa wakazi waishio sehemu za miinuko, Mahundi alisema upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama wilayani humo ni wastani wa asilimia 56.8.

Mahundi alisema ili kuboresha huduma hiyo kwa wananchi serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mipya ya Kagenyi –Omukalinzi na Mabila.

Waziri Mahundi alisema ujenzi wa miradi hiyo utahusisha ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 7.2, matenki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 105,000 na vituo 6 vya kuchotea maji.

"Utekelezaji wa miradi hii umefikia asilimia 70 na umepangwa kukamilika mwishoni mwa Juni, 2022. Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuajiri wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya Runyinya –Chanya, Kimuli – Rwanyango na Nyamiaga – Nyakatera,"alisema.

Pia alisema mradi huo utahusisha ujenzi wa matangi matano yenye ujazo wa lita 1,700,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 86.1 na ujenzi wa vituo 146 vya kuchotea maji na utakamilika Machi, 2023.

# Mkakati kufikisha umeme vitongoji vyote waja

SERIKALI imekuja na mpango kabambe wa kufikisha umeme kwenye vitongoji 37,760, ili kufika mwaka 2025 kuwe na nishati hiyo.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema hayo jana Bungeni mjini hapa wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalumu, Sophia Mwakagenda, aliyetaka kujua ni lini serikali itapeleka umeme kwenye vitongoji.

Aidha, Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Massay, katika swali la msingi, alitaka kujua lini serikali itahakikisha vitongoji vyote vina umeme, hali iliyomlazimu Waziri kutoa ufafanuzi zaidi.

Makamba alisema takwimu zinaonyesha kuwa vijiji 12,345 kati ya hivyo asilimia 80 vina umeme na vilivyobaki vitapata umeme ifikapo Desemba, mwaka huu. Pia alisema kuna vitongoji 64,760 na kati ya hivyo 37,610 sawa na asilimia 58 havina umeme.

"Manufaa ya umeme si kufika kijijini bali ni kuwafikia watu. Ili vitongoji vyote vipate umeme tunahitaji Sh. trilioni 7.4 na tumeangalia mahitaji ya miundombinu na kubaini ni lazima tuje na mpango makakati,"alisema.

Kwa mujibu wa Makamba, kwa kutumia fedha za REA, itachukua miaka 23 kwa kila Sh. 100 inayotozwa kwenye lita moja ya petroli ambayo ni njia mojawapo.

Nyingine ni ndani ya miaka minne lazima kutenga bajeti ya Sh. trilioni 1.8 kila mwaka na ya tatu kuwa na hati fungani ya nishati vijijini kwa kuhifadhi fedha zinazotokana na tozo ya petroli itakayohifadhiwa kwa miaka 20 ili zipatikane Dola za Marekani bilioni 3.1 ambazo zitapelekwa sokoni na kupata fedha.

Nyingine ni kampuni kubwa zinazoweza kupeleka umeme vijijini kuja na mpango wa kupeleka umeme kwenye vitongoji kwa miaka minne.

"Tukishakamilisha uchambuzi tutakuja bungeni kueleza ni mbinu ipi tunakwenda nayo. Dhamira yetu ni ikifika 2025 kila kitongoji kiwe na umeme wabunge wasisumbuliwe kwa suala la umeme,"alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Arumeru Mashariki, Danielson Pallangyo, alitaka kujua ni lini serikali itaunganisha umeme wa REA kwa wananchi wa vijiji vya kata za jimbo hilo.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema jimbo hilo lina kata 26 na vijiji 90, kati ya hivyo 12 havina umeme na sasa vinapatiwa umeme kupitia mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili unaotekelezwa.

"Kazi zinazofanyika sasa ni usanifu wa kina, upimaji, uandaaji wa michoro na ununuzi wa vifaa, unahusisha ujenzi wa njia za umeme ya msongo kilovoti 33 zenye urefu wa kilomita 40.30; kilomita 12 ya njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4; ufungwaji transfoma 12 za KVA 50; pamoja na kuunganisha wateja wa awali 264.

Alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 2.071 na utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka 2022.

Kuhusu gharama za kuunganishiwa umeme zilizouliziwa na baadhi ya wabunge, alisema kwa vijijini kwa njia moja ni Sh. 27,000 na mjini ni kuanzia Sh.300,000 kutegemea na umbali.




**Habari zote: Salome Kitomari na Augusta Njoji, DODOMA**



Ukurasa 12

BIBI SARA ASIMULIA JIJI MBEYA LILIKOTOKEA...



Ukurasa 13

Watanzania tuache kuendekeza masihara haya!

# BUFE

IJUMAA FEBRUARI 4, 2022
Nipashe

MIAKA 60 YA UHURU



Ukurasa 14

MKUU MAGEREZA: SASA TUNAJILISHA 90%

# Mtaalamu ujasiriamali na darasa la kuendelea kupitia usomaji vitabu



Mtu akisoma kitabu. **PICHA: MAKTABA**

IMEELEZWA kuwa mbinu za kufanikiwa kimaisha ni kuwekeza katika kusoma vitabu mbalimbali. Hapo nafasi ya uelewa kuhusu stadi za ujasiriamali nazo zina nafasi zake.

Kinadharia inaelezwa, pasipo kutumia mbinu na stadi mbalimbali za kujifunza, ni ngumu kwa mtu kubadilika kimaisha, ananena Mkurugenzi Mtendaji katika Taasisi ya Uongozi na Ujasiriamali (IMED), Dk. Donald Olomi, wakati wa uzinduzi wa kitabu kiitwacho 'Anza Kuwa na Stawi'.

Dk. Olomi alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo wa kitabu kilichoandikwa na Prosper Magali, ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wadau wa Nishati Jadilifu Tanzania (TAREA), pia Mkurugenzi wa Ubunifu na Uendelezaji Mradi wa Ensol (T) Ltd.

Dk. Olomi, ambaye yumo katika Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Elimu, anasema kazi ya maboresho ya mitaala bado inaendelea na watu waliianza mwaka 2015 kukiwapo mtazamo unaojumuisha dhana ya ujasiriamali.

"Changamoto ipo katika suala la elimu ambayo wapo baadhi ya wanafunzi wanamaliza darasa la saba hawajui kusoma na kuandika," anasema Dk. Olomi, anayeongeza kunatakiwa kuwapo shule za mfano ambazo wanafunzi watafanya kitu na kinaonekana.

Kuhusu biashara, Dk. Olomi anafafanua kuwa kawaida mtu anaanza na mtaji mdogo na baadaye anafika hatua ya mbali kibiashara, kinachomsaidia mbinu anazojifunza kukuza ujasiriamali, pia kukuza usomaji vitabu mbalimbali vya ujasiriamali.

"Nchi imepiga hatua baada ya kuwasaidia watu njia mbalimbali za ujasiriamali," anasema, akifafanua kuwa nafasi ya familia katika malezi inatakiwa vijana wajengewe uwezo katika masuala la ujasriamali.

Akizungumzia mfumo wa kisera na sheria uliopo, anasema kwanza mtu anatakiwa awe na kumbukumbu katika biashara zake, kwa maana ya 'mali bila daftari hupotea bila ya habari' na kuna mbinu zinatakiwa kuangaliwa na serikali, ili mtu aweze kulipa kodi pasipo na bugudha.

Anamtaja mwandishi wa kitabu - Magali, amekiandika ili kitakaposomwa na watu mbalimbali, kiwasaidie kubadilika ikianzia na hisia zao hadi matendo.

Pia anasisitiza umuhimu wa watu kupata fursa ya kusema na kutenda, ikiwa ni namna ya kuwawezesha kukua na kustawi kibiashara na kiuchumi, akitaka kila mtu apambane kwa kuanzia kiasi kidogo cha fursa na mtaji alio nao, ili aweze kujiendeleza kimaisha.

Rai yake ni kwamba vyema mtu akajiwekea mkakati hata anapofikia hatua ya umri wa kustaafu, awe na mbadala unaomhudumia kimaisha na sio kuhangaika upya.

Anaongeza kuwa watu wengi wanamaliza masomo katika vyuo, lakini hawana ajira rasmi, pia kundi kubwa halipo katika sekta yoyote rasmi.

"Ili kupunguza tatizo la ajira ni lazima kuwasaidia waweze kukua na ustawi," anasema Dk. Olomi, akielimisha hata wafanyabiashara wakubwa wa sasa, walianza na ujasiriamali ngazi ya chini.

Anaongeza kwamba inatakiwa kukuzwa vipaji vyao, ili waweze kunufaika na fursa zilizoko katika jamii zao.

**USHUHUDA GEREJI**

Rashid Hamza Nzowah, Mkurugenzi Mtendaji kutoka Gereji ya Nzowah, anasema siri ya mafanikio yake ni uaminifu katika kazi za wateja wake, jambo linalokuwa na mvuto kwa wateja tajwa.

"Nimekuwa mwaminifu, pamoja na kuwa na watumishi katika kampuni yangu, mimi nafanya kazi za kampuni hata nikipigiwa simu usiku wa manane naenda kufanya kazi," anasistiza.

Rashid anasema alianza kujifunza ufundi gereji mwaka 1996, huku jioni akihudhuria madarasa katika vya Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na baada ya kumaliza masomo, aliweza kufungua gereji yake iitwayo Nzowah, iliyoko Ilala jijini Dar es Salaam na kuajiri vijana 18.

Anasema gereji hiyo sasa iko katika ubora wa gereji 20 zilizoko zinazotajwa nchini. Rashid anafafanua: "Gereji yangu imesajiliwa ya kisasa kati ya gereji 20 za Tanzania zilizo bora."

Rashid anashauri watu wasikate tamaa, bali kinachotakiwa ni kujituma kwao katika kazi, ikiendana na uaminifu.

UCHUMI

# BIBI SARA ASIMULIA JIJI MBEYA LILIKOTOKEA...

- Chimbuko lake ni paliko sasa Hospitali ya Rufani
- Mabatini; wakimbizi 'Sauzi' waliezekea madebe
- Chemli, karabai; gari adimu tena Land Rover 109
- Majengo, Ghana, Soko Matola, 'Orofea' na Mafiat
- Safari Dar kwa basi DMT, ujipange, kisha TAZAMA, TAZARA...

**Na Christina Mwakangale**

MTU anapokuwa leo katikati ya Jiji la Mbeya, magari yanapita kila kona, majengo makubwa, kisha akarejesha picha zama nchi inapata uhuru, ni simulizi tofauti kabisa. Ikisikika gari ni ya serikali, aina ya Land Rover 109, tena inamchukua mtu kutembea umbali mrefu kuisikia hata zaidi ya robo saa kuiona gari.

Ni maajabu kuona kilichojiri zama hizo na sasa, masalia yaliyoko ni majina maarufu na makongwe ya mitaa, barabara, shule na ofisi au taasisi za umma.

Yapo ambayo kijamii yametoholewa kwa namna yao, ili mradi wenyeji waweze kuyatamka. Majina ya Kiingereza yaliyoachwa na wakoloni kama vile 'Orofea' kutoka Welfare Hall (ukumbi wa mkutano wa umma) ikaenga jina la eneo.

Haina tofauti an Mafiat ambako palikuwa maarufu kuegesha malori ya mizigo hasa aina Fiat yaendayo na kutoka Zambia hasa kubeba shaba, ikaibatiza; vivyo hivyo Kwa Mama John, ambako muuzaji maarufu wa vinywaji vya kienyeji, ambaye naye badaye akacha alama ya jina.

Udadisi wa Nipashe kwa wakazi wakongwe takribani zaidi ya miongo mitano, wana simulizi namna ilivyokuwa Mbeya ya kipindi hicho, wakibainisha sehemu chache zilizoacha alama ya enzi hizo, mfano Shule ya Msingi Majengo, Sisimba (zamani Market School).

Akizungumza na Nipashe, Sara Kyoga Masulu (60) mzaliwa wa Mbeya, anasema anachoshuhudia sasa vingi ni vipya ikilinganishwa na miaka ya 1960.

Anataja ushuhuda wa mabadiliko kwenye maeneo elimu, afya, shughuli za kiuchumi, makazi, miundombinu, usafiri huku akikumbuka wakazi wa mji huo walikuwa wachache sana.

Hapo anawataja watoto akiwamo yeye walioenda kwenda shule bila viatu, tena umbali mrefu na maisha ya kutumia taa za chemli na kuishia kuziona taa za karabai kwa jamii ya Wahindi waliokuwa wametoka kiuchumi.

"Nilipokuwa nakatiza mitaa ya Uhindini nikitokea Majengo nyumbani (kwa wazazi wake), nilishuhudia katika maduka ya Wahindi asubuhi mapema mmoja wa Wahindi akisafisha kioo cha taa ya karabai, iliyokesha usiku kucha.

"Yalikuwa maandalizi ya kuitumia karabai hiyo usiku, baada ya kukucha taa hizo ziliandaliwa mapema. Nyumbani tulitumia taa ya chemli ambayo aidha ilisafishwa na baba mwenyewe au mama, lakini baba zaidi, mama alikuwa si mkaaji wa nyumbani, alikuwa anaishi shamba kwenye mashamba ya mpunga Usangu.

"Baba alisafisha taa mwenyewe kwa sababu, ukimpa tu mtoto na kioo kikapasuka, utakipata wapi? Spea zilikuwa adimu na kama binti au kijana wa makamo ya ujana ukipewa uisafishe hiyo taa, utatafuta pa kulala siku hiyo, maana viboko vyake!" Anasimulia Bibi Sara.

Anasema mji huo, ulianzia palipoitwa Kiwanja Ngoma (iliko Hospitali ya Kiwanja Mpaka hivi sasa), Majengo, Mabatini na kwamba maeneo ya Jacaranda na Forest yalianza kugaiwa kwa wakazi waliohitaji makazi baada ya maeneo ulikoanzia mji kujaa.


"Eneo la Mabatini jina lake lina uhalisia mji ulikuwa wa mabeberu matupu, ambao ulikuwa mji wa makambi kwa ajili ya wapigania uhuru waliofika kutoka Afrika Kusini.

Madebe ambayo yalikuwapo zamani yalikatwa vizuri, moja moja na kisha kugeuka paa, yalihitajika madebe mengi hadi paa lote lienee.

"Ceiling board ilikuwa ya mianzi. Mianzi ilitandikwa karibu ili kipande cha debe kikija kukaa kusiwe na uwazi. Ulikandikwa udongo ambao ni imara hadi sasa nyumba hizi utazikuta Majengo na Ghana.

"Kipindi hicho bati hazikuwapo kama sasa, wala kiwanda, watu wakabuni madebe ndio mabati. Maisha ya mitaa ya zamani ilikuwa imepangwa vizuri tangu alipokuwapo mkoloni ilinyooka, akisimama mtu nyumba ya kwanza hadi ya mwisho ulikuwa unamwona," anasimulia Bibi Sara.

INATOKA UK.13



Mabatini, eneo kongwe lenye historia ya jiji Mbeya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MAENEO NA MITAA**

Kuhusu mitaa tofauti ya mkoa wa Mbeya, Sara anaitaja ilikuwapo tangu zama hizo. Inajumuisha barabara maarufu ambayo ina majina ya barabara ya kwanza hadi saba, eneo la Soko Matola.

Anaitaja mitaa hiyo wa kwanza ni iliyoko sasa Shule ya Sekondari Wasichana Loleza, mtaa huo ni Ali Hassan Road, Club Road, Amri Abeid, Malawi Road, Bahati Road na Joka Road.

"Mito inayouzunguka mji huu hadi sasa tangu awali ipo vilevile na inatiririsha maji kama zamani, isipokuwa baadhi imepunguza maji au uchafu kuziba.

"Sijawahi kushuhudia Mbeya kupata mafuriko, labda mto kuvuka kingo zake. Pengine ni kutokana na jiografia yake ya milima na mabonde. Yaani mvua ikinyesha hata muda wa saa sita, muda mfupi maji yamekauka yote yako mtoni," anaeleza Sara.

Analitaka eneo la Jacaranda, umaarufu wake unatokana na kujaa miti aina ya 'mijacaranda' na kwamba hata eneo la sasa Forest, linatokana na msitu mkubwa uliojaa miti iliyopandwa na serikali.

"Ulikuwa ukigaiwa kiwanja Forest ya zamani, ilibidi ukate miti na kung'oa visiki ili ujenge, kulijaa miti. Na Meta Hospitali ambayo ni ya wazazi hivi sasa, ilikuwa ya Baptist na Wamarekani, kwa jili ya Kifua Kikuu (TB)," anaeleza.

Bibi Sara anaeleza kuhusu eneo lililotajwa awali la 'Orofea' kama ilivyofahamika, ndiko sasa kumejengwa Uwanja wa Mkapa ambao ni maarufu kwa mikutano na sherehe mkoani Mbeya, ukiwa chini ya serikali.

"Maeneo mengi maarufu ni LEGCO ambako ilikuwa klabu ya pombe, walikutana watu maarufu tofauti kujipumzisha, na sasa imejengwa shule ya sekondari," anasema.

**USAFIRI ULIKUWAJE?**

Kuhusu usafiri kama ilivyokuwa kwa mikoa mingine, Sara anasema wakazi wa Mbeya walitumia aina tofauti, kwa ajili ya kuvuka mkoa mmoja hadi mwingine.

"Ukitoka na treni (Dar es Salama) asubuhi utafika muda ule ule ni mwendo wa saa 12. Wakati huo, kabla ya Zambia kupata uhuru mizigo yao ilikuwa inapitia bandari ya Afrika Kusini, lakini baada ya uhuru, Zambia walikuwa wanapitisha mizigo yao Bandari ya Dar es Salaam.

"Tanzania na Zambia waliunda kampuni yao iliyokuwa inaitwa Zambia Tanzania Road Services, ambayo kituo chao ilikuwa pale Ubungo Maziwa (Dar es Salaam). Baadaye ikajengwa reli ya Tanzania Zambia Railways Authority (TAZARA) ambayo waliungana nchi mbili kuomba mkopo tena katika Benki ya Dunia, lakini benki ilisitisha ombi lao la mkopo, ikabidi Mwalimu Nyerere akaenda kwa Wachina na kukubali kujenga reli hii ambayo ipo hadi sasa.

"Baadaye ilikuja shida ya mafuta, ambayo yalikuwa yanasafirishwa kwa magari, lakini wakawaza na kuja na mpango wa kujenga bomba la mafuta TAZAMA wakaomba mkopo tena Benki ya Dunia na wakakubaliwa," anasimulia.

Sara anasema kuhusu usafiri, ilikuwa ni kutwa nzima na kwamba abiria ukitoka asubuhi Dra es Salaam, unafika Mbeya asubuhi na kama ukiondoka jioni na basi utafika jioni na usafiri ulikuwa wa saa 12.

"Stendi kuu ya mabasi Mbeya ilikuwa pale Soko Kuu, Uhindini hapo ndipo ilikuwa stendi ya mabasi yote yanayotoka Dar es Salaam kuja Mbeya na kutoka Mbeya kwenda mikoa mingine jirani," anafafanua.

Anaeleza mpangilio wa barabara mjini Mbeya, akiwa na kauli: "Barabara ya kutoka Uyole hadi kupita kituo cha Esso ilikuwapo kwenda stendi kuu na kuja kutokea Mabatini na baadaye kushuka Nzovwe kuelekea Zambia.

"Ila hii ambayo ipo sasa hivi ilijengwa baada ya Uhuru, kwa sababu ilikuwa ni msitu na palitwa Forest ambalo ni jina lipo hadi sasa."

INAENDELEA UK.14



Mandhari ya jijini Mbeya kulivyo sasa.

TAFAKURI YA MLALAHOI



## Watanzania tuache kuendekeza masihara haya!

**Na Joseph Kulangwa**

KUNA mcheza soka aliyeondoka nchini kwenda nchi moja ya kiarabu kusakata kabumbu, akiaminiwa kuwa mchezaji nguli kuliko wengi nchini, tena akicheza katika klabu kubwa, lakini hamad ikasikika amerejea nchini katika klabu yake.

Waliomfuatilia wakasema kiwango alichoonyesha akiwa nchini, hakikufua dafu kwa wenzetu Waarabu, hivyo akakaa benchi mpaka waajiri wake wa awali walipomwona na kwenda kumwokoa na kadhia hiyo na sasa yuko nchini akicheza.

Lakini, tangu arejee wanasema hajaonyesha kiwango alichokuwa nacho kabla hajapanda 'mwewe' kwenda Arabuni huko kucheza. Hivyo, wapo waliosema alikwenda kutalii na sasa karudi kusimulia utalii aliouona katika nchi hiyo.

Pia, kuna usemi kwamba mzazi aliamua kumwondoa kijana wake katika shule ya msingi ya Kayumba, akitaka umaarufu akamhamishia katika shule ya Kiingereza, wenyewe wakiita Intaneshino, ambako ni umombo kwa kwenda mbele.

Na alifanya hivyo, kwa kuwa anamudu malipo ya shule hiyo ya kimataifa na hivyo alitamani kuwa uwezo wa fedha uje kuonekana katika matokeo ya kijana wake katika kutawala Kiingereza na masomo yote yafundishwayo katika shule hiyo.

Lakini, kinyume cha matokeo kijana alijikuta akifeli kila somo kuanzia la Kiingereza mpaka la Kiswahili na yote akiambulia sifuri na kuonekana miongoni mwa watoto hata wakiwano wa masikini waliojibana, ili kupata elimu hiyo, kuwa si kitu.

Hiyo ikawa ni aibu kwa mzazi ambaye alipanga kupamba ndimi za wakazi wa jamii hiyo, kuwa ana kijana anasoma Intaneshno na anaongoza darasani, lakini akajikuta anaambulia aibu kwa kijana wake. Alidhani fedha ni akili kumbe akili ni fedha.



NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

Hayo yamejitokeza nchini katika medani ya kisiasa, hivi karibuni tulikuwa na kinyang'anyiro cha kumpata Spika wa Bunge, baada ya Job Ndugai, alipojikuta akijiuzulu ghafla kutoka shinikizo kutoka kwa wenye nchi yao.

Sasa katika kinyang'anyiro hicho, ndipo paliibuka futuhi ya aina yake, wapoibuka watu kwanza ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho ndicho kilikuwa na Spika aliyejiuzulu, wakitaka kuziba pengo hilo la kiongozi wa mmoja wa mihimili mitatu ya Dola.

Watu 71 kwa kuwa walikuwa na uwezo wa shilingi milioni moja, wakanunua fomu wakijiaminisha kuwa wangeweza kukalia kiti hicho kilichopata kukaliwa na Erasto Mang'enya, Adam Mkwawa, Pius Msekwa, Samuel Sitta, Anne Makinda na Ndugai.

Yaani idadi ya waliojitokeza kulimfanya mtu makini kutanua jicho la uchunguzi, maana ni wengi kana kwamba walikuwa wanatafuta kiranja mkuu wa shule au wa darasa.

Lakini, wakati mshangao huo ukiendelea, ndipo mchujo ukaingia bungeni kwenyewe kutoka vyama mbalimbali vya siasa, huku chama kimoja tu ndicho kikiwa na mbunge akiwania nafasi hiyo ya juu nchini.

Wengine wakawa kama wasindikizaji abiria kituo kikuu cha mabasi Magufuli, Dar es Salaam. Baadhi hata kujua walikuwa wanawania nini, wakawa hawajui na hata walipoulizwa wakajikuta wanaweweseka, kuwa hilo jambo liliwakuta mikoani wakinunua au kuuza mazao!

Wengine tukawasikia wakilalama eti wakipewa uspika siku wanachaguliwa tu, neema ingeshuka katika Mjengo. Mjengo wenye watu makini wakiwakilisha Watanzania milioni 60!

Tukashuhudia Bunge likigeuzwa kijiwe cha watu kujitangaza kujulisha ndugu zao kuwa wako mkoa gani nchini na wanachama wa vyama vipi. Wakitumia jukwaa hilo kuhanikiza kwa ndugu hao wakiwajulisha kuwa nao wapo nchini na ni maarufu wawezao kuongoza Taifa hili.

Matokeo ni hatimaye mgombea wa CCM akaibuka na ushindi wa asilimia 100 na kuwagawia wale wanane wengine sifuri, sifuri! Lakini walioshindwa wakashangilia kuwa angalau wamejulikana, angalau wamekanyaga zuria la Bunge na angalau wameonekana na kusikika kwenye vyombo vya habari.

Hayo mambo yanayogusa hisia zetu, ni wazi inatukumbusha kuwapo makini hata tukachagua viongozi watata katika mihimili hii mitatu muhimu ya dola, kwa sabau sasa wapo wanaofanya nafasi ya uongozi kama utani, baadhi yetu tunasimama kwa namna kutamba nao. Tukimuendekeza nyani, tutavuna mabua. Alamsiki!

FEDHA

# MKUU MAGEREZA: SASA TUNAJILISHA KWA 90%

## SHIRIKA NALO LANG'ARA MIRADI ULINZI, UZALISHAJI MAONO YAJAYO KUWA NA JESHI LINALOJITEGEMEA

**Na Renatha Msungu DODOMA**

LILIKUWA agizo la Rais Dk. John Magufuli, kwa Jeshi la Magereza lijitegemee kiuchumi. Leo hii, linatangaza kufanikiwa kwa zaidi ya asilimia 90, kupitia uchumi wa kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Hata sasa imefikia magereza yanajilisha

Baada tu ya kuingia madarakani, Kamishna Jenerali Suleiman Mzee, aliweka mkakati wa kulima mazao ya chakula na biashara, pia miradi inayofanikisha kulibadilisha jeshi hilo katika uchumi kupitia sekta zote inazohudumia.

Kamishna Jenerali Mzee, anasema alitathmini mwenendo wa kazi za jeshi lake, kisha akatathmini juhudi za wakuu wa kitengo wenye sifa, akawakabidhi ukuu wa gereza.

Sasa anakiri manufaa leo akitaja imeweza kuokoa deni la bajeti ya Sh. bilioni 29 za chakula kulisha wafungwa na walioshikiliwa kila mwezi, kwa hesabu ya watu zaidi ya 31,000 kitaifa.

### KAMISHNA JENERALI MZEE

Kamishna Jenerali Mzee, anasema jeshi hilo lilipewa fedha Sh. milioni 800 kwa ajili ya chakula, huku kujitegemea kwao katika kilimo kumeokoa Sh, bilioni 29 walizotumiwa kwa mwezi huo kwa ajili ya kulisha wafungwa 31,000, zilipata mbadala wa matumizi .

Anasema hadi sasa hakuna tena madeni ya wazabuni wa kila mwezi wanaolisha wafungwa magerezani, kwa sababu wanajitegemea kwa mlo.

Kamishna Jenerali Mzee, anasema wanajitegemea kwa asilimia 90, akifafanua:

"Hivi sasa fedha Sh.milioni 800 za chakula kwa mwezi ambazo zilitolewa na serikali kwa

ajili ya chakula, zinakwenda kufanya kazi nyingine."

Anataja mazao wanayozalisha yanajumuisha mbegu za kutosha za alizeti, mahindi na maharage, ili kuepusha uhaba msimu wa kilimo unapowadia katika Magereza mbalimbali nchini.

Hapo Afande Mzee anajisifu kwamba kwa miradi ya kilimo cha mazao ya chakula wapo vizuri, kila gereza wanajilisha, huku wakifanikiwa kulipa madeni yote ya wastaafu 500 waliokuwa wanawadai na sasa

hakuna deni kwa wastaafu hao.

Kamishna Jenerali Mzee anataja pia miradi mingine ikiwamo ya matofali yanayotumika kujenga nyumba za watumishi, pia wanayauza kwa jamii, akijivunia kuhakikishiwa kutekeleza majukumu ya Magereza kwa ufanisi, ikiwamo mradi wa ujenzi nyumba za watumishi.

Anataja mradi mwingine wa mashine, fremu za duka, kiwanda na mradi matofali, pia kilimo, vyote anavijumuisha kuwa ni hazina kubwa kwa jeshi hilo, kwa sababu zina manufaa makubwa.

Kamishna Jenerali Mzee, anasema lengo lao ni kuona Jeshi la Magereza linajitegemea kwa kila kitu; chakula, mavazi na mahitaji yote ya msingi.

### SHIRIKA LA MAGEREZA

Mkurugenzi wa Shirika la Magereza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Justine Kaziulaya, anasema SHIIMA iko mstari wa mbele kwa sababu wana kila kitu muhimu ndani ya shirika hilo mali ya Magereza.

SACP Kaziulaya, anataja kampuni walizo nazo ni za ulinzi, usafi na nyingine nyingi zinazojishughulisha na kazi mbalimbali kitaifa, huku akikiri mageuzi ya afande wake Kamishna Jenerali Mzee.

Anataja eneo mojawapo la mabadiliko makubwa, ni pamoja na jeshi hilo kuanzisha miradi ya kilimo na biashara yanayolisaidia jeshi kufanya shughuli zake kwa ufanisi.

Anatolea mfano, hivi sasa wanaendesha miradi ya biashara inayowaingizia kipato kikubwa na ambacho kinatumika katika shughuli mbalimbali.

Pia, SACP Kaziulaya, anaitaja kampuni ya ulinzi inafanya vizuri sana katika kazi zake, kwa kupata tenda mbalimbali za kulinda wakiwa na sifa kubwa kutokana na walinzi waliofuzu kwa ufanisi wa kutosha.

Wito wake ni kwamba, serikali iwape ushirikiano kibiashara katika kufanikisha majukumu yake, akifafanua timu yao inaundwa na walio kifungoni na askari, wakiwa katika ushirikiano mkubwa.

Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Keneth

Mwambije, anawapongeza wakuu wa magereza mkoani humo kutokana na kazi

za miradi wanayoiendesha mikoani huku, akiungana kukiri ni zao la kazi ya mageuzi kutoka kwa Kamishna Jenerali Mzee ambaye, amehakikisha kila gereza

linapata mahitaji stahiki ya kuendesha miradi waliyokabidhiwa.



Kamishna Jenerali wa Magereza, Suleiman Mzee. **PICHA: MTANDAO.**

> **"SACP Kaziulaya, anataja kampuni walizo nazo ni za ulinzi, usafi na nyingine nyingi zinazojishughulisha na kazi mbalimbali kitaifa,**

INATOKA UK.12

# BIBI SARA ASIMULIA JIJI MBEYA LILIKOTOKEA...

BARABARA YA DAR

Mkongwe huyo wa jijini Mbeya anasimulia, barabara ya kutoka Dar es Salaam kupita Mikumi pia haikuwapo, bali msafiri wa gari kutoka Mbeya au Dar alipitia Kilosa kutokea mjini Morogoro ndipo na kuunganisha na jijini Dar es Salaam.

"Mikumi lilikuwa ni pori la wanyama na baadaye ikajengwa barabara hiyo ya moja kwa moja toka Dar es Salaam hadi Mbeya-Tunduma, baada ya uhuru, ili kurahisisha usafirishaji mizigo na abiria.

"Usafiri wa TAZARA, watu walikuwa wanasafiri na vyakula pia wapishi wa treni nao walikuwapo kwa wale wanaopenda kwenda kula katika hoteli ya treni," anaeleza.

Anataja eneo maarufu la Mafiati jijini Mbeya, ilikuwa ni kituo kikubwa cha magari ya mizigo makubwa yanayoenda Zambia na kusubiri hapo, ili kupakia mizigo ya kwenda nayo nchi jirani.

"Umbali wa kutoka Dar es Salaam mpaka Mbeya ulichukua muda wa siku mbili, ambao ukiondoka leo Dar es Salaam au Mbeya usiku saa nne, utafika saa nne tena usiku. Mabasi yalikuwa yanaitwa DMT (Dar es Salaam Motor Transport) ikaja KAMATA (Kampuni ya Mabasi ya Taifa ) na magari mengine mengi (kama ya Shirika la Reli Tanzania - TRC) yalikuwapo ya watu binafsi miaka 1970 na kuendelea," anaeleza.

UJASIRIAMALI CHAI

Sara anasimulia akiwa binti mkubwa wa familia ya watoto kadhaa, alitekeleza majukumu ya nyumbani na baba yake aliyekuwa mpika chai maarufu katika Soko Kuu, yeye ilimlazimu kujitwisha kapu la maandazi kila alfajiri kumpelekea baba sokoni.

"Mama alipika maandazi aidha usiku kabla ya kulala au alfajiri, baba alipoamka asubuhi alitoka kuwahi kchesha chai sokoni, vitafunio mimi nilimpelekea. Wateja nilikuwa nawaona wengi na shughuli hiyo ya baba ilitufanya tuishi maisha mazuri tu, nyumba nzuri yaaani kwa kifupi tulikuwa watoto wa 'kishua," anasimulia.

Bibi Sara anaeleza maisha ya baba yake mpishi wa chai, wameyarithi baadhi ya watoto wa kike, yeye ambaye baada ya kuwa mtu mzima, na kuhitimu Chuo cha Usekretari Magogoni (Dar es Salaam), akaajiriwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wakati huo.

Sara anasema akaona mshahara hautoshi, naye akaanza kufanya shughuli kama ya baba yake, ingawa ilikuwa ya kisasa zaidi, akifafanua: "Kwa upande wa familia yetu tuliorithi zaidi shughuli hii ni wawili.

"Dada yangu mkubwa na mimi. Ilifika wakati nilipoajiriwa benki, niliamua kuacha kazi, niliona muda ninaopoteza ofisini ikilinganishwa na kipato cha mwezi ni kidogo kuliko biashara yangu," anaeleza Sara.

Anasema amefanya biashara ya mgahawa katika mikoa tofauti na kipato cha biashara kilimsaidia kujiinua kiuchumi, hata akaweza kumiliki mali kadhaa.

"Baba yangu alifariki mapema, naweza kusema hivyo nikiwa na umri wa miaka kama 24. Nilishakuwa na familia yangu, ila naweza kusema majukumu niliyoshuhudia baba akiuza chai yamechangia kwa kiasi kikubwa kufahamu umuhimu wa kujiajiri," anabainisha.



# DC: Wanawake kuweni majasiri kwenye uongozi

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

MKUU wa Wilaya ya Kondoa, Hamis Mkanachi, amewataka wanawake kuwa na ujasiri na uthubutu wa kuwania nafasi za uongozi ili kufikia lengo la usawa wa 50 kwa 50.

Mkanachi aliyasema hayo alipokuwa akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake katika masuala ya usawa wa kijinsia, uongozi na ushirikishwaji, wilayani humo.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Women Wake Up (WOWAP) na kushirikisha madiwani wanawake kutoka Wilaya za Bahi, Kondoa, Mpwapwa na Kongwa.

Alisema wanawake wanatakiwa kuwa na uthubutu katika kugombea nafasi mbalimbali za maamuzi ili kufikia lengo hilo bila kikwazo.

"Wanawake wanatakiwa kuwa na ujasiri wa kujitoa na kugombea udiwani badala ya kufikiria viti maalum tu kwa kufanya hivyo, mtakuwa mmeongeza idadi ya wanawake viongozi lazima muwe na mkakati wa kufikia asilimia 50 kwa 50," alisema.

Alisema madiwani ni viongozi walio karibu na jamii ni muhimu kama madiwani wanawake watakuwa wengi ili kuwa kichochea cha mabadiliko.

"Ukatili wa kijinsia bado ni mkubwa takwimu za kufungua zinaonyesha wanawake sita kati ya 10 wanafanyiwa ukatili na wapenzi wao, au watu wao wa karibu," alisema.

Alisema jamii inatakiwa kupunga vitendo vya kikatili na kutoa taarifa pindi wanapoona ukatili inatendeka.

Mkurugenzi wa WOWAP, Fatma Toufiq, alisema kuna mahitaji makubwa sana ya mafunzo kwa viongozi wa wanawake.

Hata hivyo, alisema bado wana kero nyingi kama viongozi katika ngazi ya jamii na kwamba mafunzo hayo yataongezea weledi.

Mratibu wa WOWAP, Nasra Suleiman, alisema shirika hilo limekuwa likifanya kazi ya utetezi kwa wanawake na watoto lengo ni kuona jamii isiyo na ukatili kwa wanawake na watoto.

Pia alisema limekuwa likitekeleza miradi mbalimbali ya kupinga ukatili, ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni.

Aliwataka wananchi kushirikiana kukabiliana na vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia hususan ukeketaji, ambao unaendelea kufanyika kwa siri.

# Mangula: Mikutano iwe suluhisho la kero

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Philip Mangula, amewataka viongozi na wanachama kutumia mikutano ya ndani kuzungumza na kupata suluhu la kero zinazowakabili.

Mangula alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na wanachama pamoja viongozi wa chama hicho kwenye maadhimisho ya miaka 45 ya kuzaliwa kwa CCM kimkoa yaliyofanyika katika Kata ya Bumbuta wilayani hapo.

Alisema wanachama na viongozi wakikutana na kuongea mara kwa mara ndiko kutasaidia kukijenga chama.

"Muwe na utaratibu wa kukutana kila wakati na kuzungumza kwani kuna kero na mambo mengi ya kuongea yanayohusu chama chetu cha Mapinduzi na jambo kubwa niwasisitize mnapokutana usidharau jambo la mtu akileta jambo lichukue na kama kiongozi lifanyie kazi," alisisitiza Mangula.

Aidha, aliwataka wanachama wa CCM kudumisha amani na utulivu wa nchi kwa kuwa bila amani Taifa haliwezi kufanya shughuli yoyote ya kuleta maendeleo.

"Hivi karibuni tumesikia mauaji ya watu yakitokea katika mikoa yetu, sasa kama viongozi wa chama mkae na mkutane kwenye vikao na kutolea ufafanuzi mambo haya ya mauaji kwa maslahi ya chama na wananchi wetu kwa ujumla," alisema Mangula.

Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Pili Mbaga, alisema chama hicho kinalaani matukio ya mauaji ambayo yametokea hivi karibuni.

"Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma kinalaani mauaji ya wanawake wawili na wengine watano wa familia moja waliouawa katika kijiji cha Zanka, ambapo chanzo kilichohusishwa na matukio hayo ni wivu wa mapenzi na kulipizana visasi na kutoa wito wananchi kutoa taarifa kwa wageni wanaowatilia shaka katika maeneo yao," alisema.

Naye Mbunge wa Kondoa Vijijini ambaye ni Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema wanajivunia mafanikio ya chama hicho yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 45, ambapo wakati chama hicho kinazaliwa jimbo hilo halikuwa na shule ya sekondari hata moja wala kituo cha afya.

Alisema hadi sasa jimbo hilo lina shule za sekondari 26 na vituo vya afya saba na tayari serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya kuongeza kituo kingine cha afya.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (katikati), akizungumza jijini Dodoma jana, katika uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 100 ya Mwalimu Nyerere, yenye lengo la kutangaza mambo aliyofanya wakati wa uhai wake, ili kuwa sehemu ya vivutio vya Taifa vya kuutangaza utalii. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Maboresho sheria, kanuni matumizi zebaki kuendelea

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesisitiza kuendelea kufanya mapitio na maboresho ya sheria na kanuni zilizoko kwa kuingiza vipengele vitakavyosimamia uagizaji, utunzaji na utumiaji wa kemikali ya zebaki.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia mazingira, Edward Nyamanga, alibainisha hayo jijini hapo wakati wa kufungua warsha ya mafunzo kwa wakaguzi wa mazingira.

Alisema hatua hiyo ya kufanya mapitio na maboresho ya sheria na kanuni zilizoko ni katika jitihada za kudhibiti matumizi ya zebaki hapa hususani kwa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu.

Alisema Tanzania imeridhia mkataba unaotaka kuzuia matumizi holela ya zebaki, na serikali ilikuja na mpango kazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu wa miaka mitano. Nyamanga alisema katika kutekeleza mpango kazi huo, serikali ilikuja na mradi wa miaka mitano wa kupunguza au kuondosha kabisa matumizi ya zebaki kwenye uchimbaji mdogo wa dhahabu ambao unatekelezwa kwenye mikoa saba yenye wachimbaji wadogo wengi wa madini ya dhahabu.

Alisema kupitia mradi huo, utafanyika utafiti wa kiteknolojia mbadala zilizoko nchini na zile ambazo zinafanyiwa tafiti mbalimbali na kwa teknolojia ambazo zitaonekana zinafaa zitawezeshwa kifedha na kufanyiwa majaribio.

"Teknolojia ambazo zitaleta matokeo tarajiwa ya malengo ya mradi zitasambazwa kwa wachimbaji wadogo na elimu juu ya matumizi sahihi ya teknolojia hizo itaendelea kutolewa ili kuwawezesha kuondokana na matumizi ya zebaki," alisema.

Pia alisema serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi hususani wachimbaji wadogo kuhusu madhara ya zebaki na namna bora ya kutumia vifaa kinga ili kuitumia bila kuathiri afya na mazingira. Mafunzo hayo ya siku tatu yanashirikisha wakaguzi wa mazingira na migodi wapatao 60 kutoka mamlaka za usimamizi na udhibiti wa mazingira ikiwa nia pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Makamu wa Rais, Tume ya Madini, ofisi za madini kutoka mikoa saba ya Geita, Mwanza, Mara, Shinyanga, Singida, Mbeya, na Songwe.

Mafunzo hayo yamelenga kuwapa mbinu za kuboresha utendaji kazi katika kusimamia matumizi ya zebaki kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo ambapo ongezeko la wachimbaji huenda sambamba na ongezeko la matumizi ya kemikali ya zebaki.

Tathmini ya hivi karibuni inaonyesha kuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini hutumia zaidi ya tani 18.5 ya zebaki kwa mwaka ambazo hutumiwa bila kuzingatia tahadhari na kusababisha athari ya afya kwa binadamu na mazingira.



# TARURA yabanwa uharibifu barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MADIWANI wilayani Mbarali wameutaka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wilayani Mbarali kutumia sheria ndogo za halmashauri hiyo kudhibiti uharibifu wa barabara zake unaosababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo na mifugo.

Wakizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kilichoketi kujadili na kupitisha Bajeti ya Halmashauri hiyo, baadhi ya madiwani walisema barabara nyingi ndani ya halmashauri hiyo zinaharibiwa na shughuli za kibinadamu hususan kilimo na mifugo. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalib Kibadamo, alisema baadhi ya wananchi wanalima hadi kwenye kingo za barabara na kusababisha mmomonyoko wa udongo wakati wa mvua, hivyo barabara kukatika.

Alisema wilaya hiyo pia ina mifugo mingi ambayo hupitishwa kwenye barabara kwa umbali mrefu kila siku jambo ambalo linachangia uharibifu wa barabara hasa maeneo ya vijijini. Kibadamo aliitaka TARURA kutumia sheria ndogo za halmashauri hiyo kukabiliana na uharibifu huo wa miundombinu ambao unasababisha athari kubwa katika maisha ya wananchi wa wilayani Mbarali.

"Anzeni kwa kuweka mabango yanayopiga marufuku mifugo kupitishwa katikati ya barabara na wakulima kulima hadi kwenye kingo za barabara, mabango hayo yaonyeshe na faini zitakazotozwa kwa wale watakaokiuka amri hiyo kisha watendaji wetu ambao wapo huko vijijini waanze utekelezaji wa kusimamia suala hilo," alisema Kibadamo.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara, Meneja wa TARURA Wilaya ya Mbarali, Sambo Mahona, alisema kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2020/21, vyanzo vya bajeti halmashauri hiyo ni vitatu.

Alivitaja vyanzo hivyo ni Mfuko wa Barabara (Road Fund) Sh. bilioni 1.012, fedha kutoka Serikali Kuu kupitia tozo za miamala ya simu Sh. bilioni moja na fedha kutoka mfuko wa jimbo Sh. milioni 500 na kufanya jumla ya bajeti ya barabara wilayani Mbarali kuwa Sh. bilioni 2.5.

Mahona alisema kuwa kati ya fedha hizo, kati ya kipindi cha Julai hadi Desemba tayari wamefanikiwa kupokea Sh. milioni 337.4, sawa na asilimia 33 ya bajeti kutoka Mfuko wa Barabara, Sh. milioni 307.9 sawa na asilimia 31 ya bajeti kutoka Serikali Kuu kupitia tozo za simu na Sh. milioni 300, sawa na asilimia 60 ya bajeti kutoka Mfuko wa Jimbo.

Alisema mpaka sasa fedha zilizokwishatumika ni Sh. milioni 307.4 za Mfuko wa Barabara ambazo ni sawa na asilimia 100 ya fedha walizopokea na Sh. milioni 27.9 kutoka Serikali Kuu ambazo ni sawa na asilimia tisa ya fedha walizopokea huku katika Mfuko wa Jimbo wakiwa wametumia Sh. milioni 71.9, sawa na asilimia 24 ya fedha walizopokea.

Aliwaomba madiwani hao kupitisha bajeti ya Sh. bilioni 2.512 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwamo Mfuko wa Barabara, Serikali Kuu kupitia tozo za miamala ya simu na Mfuko wa Jimbo.



Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mbeya (RCC), wakiendelea kufuatilia mawasilisho mbalimbali yaliyokuwa yanatolewa na wadau kwenye kikao kilichofanyika, jijini Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# DC amulika matumizi ya fedha za mikopo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali ameitaka halmashauri ya wilaya hiyo kuhakikisha fedha za mikopo inayotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zinatumika kuanzisha miradi ya kufyatua matofali ya saruji ambayo yatasaidia wananchi kujenga nyumba bora na kurahisisha ujenzi wa majengo ya serikali.

Reuben Mfune alitoa rai hiyo jana alipokabidhi hundi ya Sh. milioni 290.8 kwa vikundi vya ujasiriamali, fedha ambazo zilitolewa na halmashauri hiyo kama mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mfune alisema kuwa mahitaji ya matofali ya saruji ndani ya wilaya yake ni makubwa kutokana na miradi mingi ya ujenzi inayoanzishwa na serikali, kukosa matofali hayo na badala yake kutumia matofali ya kuchoma. "Wakati tunajenga majengo ya serikali kama vile vyumba vya madarasa, ofisi za watendaji, zahanati au vituo vya afya, tunahitaji matofali ya saruji, lakini hatuyapati kwa vile hakuna watu wa kutosha wanaoyafyatua ndani ya wilaya hii.

"Tunalazimika kutumia matofali ya kuchoma ambayo yanasababisha tupoteze muda mwingi wakati wa kujenga, hii ni fursa kwenu vijana kutumia fedha hizi za mkopo kuanzisha mradi wa kufyatua matofali ya saruji mkijua kabisa kuwa soko lake lipo," alisema Mfune.

Alisema kuwa mbali na kusaidia ujenzi wa majengo ya umma, pia wananchi watavutiwa kuyatumia na hivyo kusababisha jamii kujenga nyumba bora na za kisasa kuliko zile za matofali ya kuchoma na mabichi.

Akizungumzia mkopo huo, Mfune alivitaka vikundi vilivyofanikiwa kuupata, kuutumia kwa malengo yaliyokusudiwa ili wazalishe na kurejesha mikopo yao kwa wakati.

"Msije mkatumia fedha hizi kwa anasa, badala yake mkafanye kazi za uzalishaji kama mlivyoomba na kisha mrejeshe mikopo yenu ili watu wengine nao wapewe, lakini mkirejesha kwa wakati mnajiweka katika mazingira mazuri ya kukopeshwa fedha nyingi zaidi na mkafanya mambo makubwa zaidi," alisema Mfune.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Roman Kessy, alisema vikundi 39 vitanufaika na fedha hizo ambazo ni asilimia 10 ya makusanyo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.

Akifafanua zaidi upatikanaji wa fedha hizo, alisema Sh. milioni 117.75 ni fedha zilizotokana na marejesho ya mikopo ya zamani na zitakopeshwa tena kwenye vikundi vingine 16.

Kessy alisema Sh. milioni 173.1 ni aslimia 10 ya makusanyo ya halmashauri kwa robo ya pili ya mwaka wa fedha inayoanzia mwezi Oktoba hadi Desemba ambazo pia zimekopeshwa kwa vikundi 20 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Kati ya fedha hizo, pia zimo Sh. milioni 20 ambazo tumezikopesha kwa kikundi cha vijana wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) cha Dreams ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge alipotembelea wilayani Mbarali," alisema Kessy.

Mkopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu unatolewa kwa mujibu wa sheria na halmashauri zote nchini kwa lengo la kuinua kiuchumi makundi hayo.

## Wananchi waiangukia serikali ujenzi mifereji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Nsalala katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuboresha mifereji ya maji ili kuepusha mafuriko kuvamia makazi yao na kusababisha madhara.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, wananchi hao walisema mifereji ya maji katika mji huo haijaboreshwa na hivyo kusababisha maji ya mvua kukosa uelekeo na kusambaa kwenye makazi, hali ambayo ni hatari.

Mmoja wa wananchi hao, Tilson Kamwela, alisema kuwa wakati wa kiangazi, ulikuwapo mradi ambao ulikuwa unatekelezwa na serikali wa kupanua mitaro ya maji, lakini mpaka sasa mradi huo haujakamilika na kwamba huo ndio uliosababisha matatizo zaidi.

Alisema maji yanajaa kwenye mifereji hiyo na kuanza kutoka kuingia kwenye makazi ya watu, hali ambayo alisema endapo watu wazima hawapo nyumbani yanaweza kutokea maafa kwa watoto.

"Maji yote yameelekezwa sehemu moja sasa yanapokutana yanakuwa mengi kiasi kwamba hayawezi kuingia yote kwenye mtaro unaoyaelekeza Mto Mbalizi, sasa badala ya kunyooka yanaanza kutoka na kusambaa kwenye nyumba zetu," alisema Kamwela.

Aliomba mfereji unaoelekeza maji katika eneo la Mapelele ukamilishwe haraka ili kupunguza maji yanayopita kwenye mfereji unaopita Kabale kuelekea machinjioni.

Monica Samwel alisema maji hayo yanaingia kwenye makazi yao yakiwa na taka ambazo baadhi ni chafu na zinaweza zikawasababishia maradhi.

Alisema baadhi ya wananchi wanatupa vinyesi na nguo chafu, hivyo kuhatarisha maisha ya watoto ambao huwa wanayachezea maji hayo.



# Juma Duni: Sina kinyongo na mtu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ACT- Wazalendo, Juma Duni Haji, amesema kuwa uchaguzi wa chama umeisha hivyo hana kinyongo na kwamba ambao hawakumuunga mkono warudi katika chama ili kukijenga.

Aliyasema hayo juzi katika ofisi za chama hicho Vuga Mjini Zanzibar wakati akizungumza na wafuasi wa chama hicho waliompokea kwa shangwe na nderemo baada ya kuwasili Zanzibar akitokea Dar es Salaam, ambapo chama hicho kilikuwa na uchaguzi wa kujaza nafasi ya uenyekiti Taifa na makamu mwenyekiti Zanzibar kufuatia kifo cha aliyekuwa mwenyekiti, Maalim Seif Sharif Hamad, mwaka jana.

Alisema kilichomlazimisha kubaki katika siasa ni jinsi watu wanavyouana kwa sababu ya uchaguzi, hivyo ni lazima kuheshimiana na kutambuana bila ya kujali mtu eneo analotoka.

Alisema kuwa hakuna kitu kinachomchukiza kama ubaguzi hasa wa Upemba na Uunguja na kama angekuwa na madaraka angefuta utabaka huo.

Alieleza kuwa hana sababu ya kuwafukuza au kuwatenga wale ambao hawakumuunga mkono wakati akigombea nafasi hiyo.

"Yaliyopita si ndwele tugange yajayo, tumeshapata mwenyekiti wa chama sasa tuna chama chenye uongozi uliokamilika kazi tuliyonayo ni kujenga chama na kutetea haki zetu ili na sisi tupate haki yetu,"alisema Duni.

Aliahidi kushirikiana na viongozi na wanachama kujenga chama na atahakikisha anafanya siasa katika pande zote za Tanzania.

"Msijiogopeshe kitu, wengine walidhani nikifika nitafukuza mtu kwanza, sina mamlaka hayo mpaka nishirikiane na chama, wale waliokosa nafasi hii rudini tushirikiane kujenga chama ili kujiandaa na uchaguzi mkuu," alisema.

Aliongeza: "Naomba msaada wenu msiniache, endeleeni kuniambia yale nisiyoyapenda maana huko ndio kurekebishwa kwa makosa ya mtu."

Naye Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Othman Masoud, ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, alisema amegombea nafasi hiyo kwa manufaa ya chama na taifa, hivyo ataitumikia nafasi hiyo vizuri.

## Wizara yapokea msaada wa vifaa tiba vya mil.92/-

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, imepokea msaada wa vifaa tiba vya mama na mtoto vyenye thamani ya Sh. milioni 92 kwa lengo la kuimarisha afya bora nchini.

Akipokea msaada huo jana huko Wizara ya Afya, Mnazimmoja Mjini Zanzibar, Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, alisema vifaa hivyo vitasaidia kupunguza tatizo la uhaba ulioko katika Hospitali za Unguja na Pemba.

Alisema ukosefu wa vifaa tiba ni jambo linalodhorotesha matibabu hasa kwa kinamama na mtoto, hivyo kupatikana kwa vifaaa hivyo ni jambo jema ambalo litasaidia jamii.


Akizungumzia kuhusu upatikanaji wa dawa, Waziri Mazrui alisema kuwa kwa sasa dawa zilizoko hazitoshelezi kutokana na wingi wa wagonjwa, lakini wanafanya jitihada zaidi kuhakikisha wananchi wanapatiwa matibabu ya uhakika.

"Upatikanaji wa dawa hazitoshelezi kutokana na ongezeko la wagonjwa, lakini tunajitahidi tuhakikishe wananchi wetu wanapata dawa angalau kwa kiasi kilichoko," alisema.

Aliishukuru Taasisi ya PhamAcces Foundation kwa kuwapatia vifaa hivyo na kuwaomba kuendeleza ushirikiano ulioko ili kuimarisha afya katika jamii.

Naye Mkurugenzi wa Pham Acces Foundation, Dk. Heri Marwa, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuimarisha afya ya mama na mtoto katika jamii.

Aidha, alisema kuwa wameamua kutoa msaada huo baada ya kufanya utafiti kwa kutumia data kupitia hospitali mbalimbali Unguja na Pemba na kugundua kuwa ipo haja ya kuongeza nguvu hasa kwa kinamama na watoto.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kushoto), akipokea msaada wa vifaa tiba kutoka kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Pharm Access Foundation, Dk. Heri Marwa, ofisini kwake Mnazi Mmoja, Mjini Unguja jana, ambavyo vitasaidia kutoa huduma za afya kwa mama na mtoto katika Hospitali za Wilaya ya Kaskazini "A" na Micheweni Pemba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Migogoro ya ndoa ilivyoathiri watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ONGEZEKO la talaka na migogoro ya ndoa imeelezwa kuathiri jamii hasa watoto na kusababisha kukosa masomo, kudhalilishwa kijinsia na kujiingiza katika ajira za utotoni.

Hayo yalielezwa na Kadhi wa Mahakama ya Kadhi Wilaya ya Kaksazini 'A' Unguja, Omar Shehe Khamis, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake Mkokotoni.

Alisema wimbi la talaka katika wilaya hiyo linasababishwa na jamii kutokuwa na elimu ya ndoa na ndoa za umri mdogo na kwamba wanaofunga ndoa wengi hawajakomaa kumudu maisha ya ndoa.

Aidha, alisema hali ngumu ya maisha pia husababisha migogoro ya ndoa na matokeo yake wanawake kulalamika kukosa haki yao ya ndoa kutokana na waume zao muda mwingi kuutumia katika kutafuta maisha. "Zipo kesi hapa zimeripotiwa na wanawake kukosa haki yao ya ndoa (unyumba) kwa sababu waume zao muda mwingi wapo katika harakati za kutafuta maisha na hawana muda wa kustarehe na wake zao,"alisema kadhi huyo.

Alieleza kuwa licha ya ugumu wa maisha, wanaume waliomo katika ndoa kuhakikisha wanatimiza wajibu wao na kuwa karibu na familia zao, ili kuepusha athari ambazo zinaweza kujitokeza ikiwamo wimbi kubwa la takala na watoto kukosa matunzo.

"Ndoa inapovunjika watoto huwa hawapati kusoma kwa utulivu maana leo yuko kwa mama na kesho yake yupo kwa baba, hivyo hupeleka watoto kuhangaika," alisema.

Naye Kadhi wa Mahakama hiyo Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, Mohammed Ramadhani Khamis, alisema ndoa za watu wa zamani zilikuwa zikidumu kutokana na wanandoa kuvumiliana na kuthamini ndoa zao tofauti za ndoa za sasa.

Alisema matatizo mengi yanayopelekea ndoa kuvunjia yanasababishwa na wanaume kushindwa kutimiza majukumu yao.

Msaidizi wa Sheria Wilaya ya Kaskazini 'B', Omar Ali Khamis, alisema udhalilishaji pia unachangia ongezeko la talaka kwa sababu badala ya kesi kufikishwa mahakamani familia mbili zinaamua kuwaozesha watoto wao wakati bado wako tayari kuingia katika uhusiano wa ndoa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI

### OMBI LA URAIA



MR ZHOU TAO

MR ZHOU TAO mwenya picha hapo juu, anaomba Uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Utaifa wake wa sasa ni CHINA Nchi atokayo CHINA shughuli zake MKURUGENZI anwani ya mwajiri S.L.P 77800 Dar es salaam. Yupo hapa nchini tangu 2008 pamoja na kuishi Dar es Salaam pia amewahi kuishi Dar es Salaam.

Kwa yeyote mwenye taarifa/ sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa kamishna mkuu wa uhamiaji S.L.P 512, Dar es Salaam.

### KUPOTEA KWA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**SONIA MMASA MSUYA** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba **TAE 273398** iliyotoLewa na wizara ya mambo ya ndani(Uhamiaji) **PCO, DAR ES SALAAM** mwaka **2020**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/CHU/RB/48661/2022.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHADOWS OF AFRICA LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T 578 AKB** chasis namba **LH1190066130**, engine namba **3L687248**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/47416/2022**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ODA ISAAC SEKIROMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T947 ATL aina ya TOYOTA VITS Chassis namba: SCP105008860, engine namba: ISZ0352701 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **DAR/MBU/RB/46996/2022.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 9 OF 2022**

In the Matter of the Estate of the Late Philipo Mgela Leonard

By 1.Gaudensia Philipo Mlangali
2. ……………………………..

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 09th day of February….. 2022
Dated at MOROGORO this 21 day of January………2022

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi……09..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU TABU A.BAJUNI WA KIHONDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SALIM RAMADHANI NYAGANGA.**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 17/02/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 03/02/2022**

### TANGAZO!!
### AFRIWELD INDUSTRIES LTD
### Nafasi ya kazi

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35
**Nafasi:** Mauzo
MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!!
wahi sasa Kupata nafasi nzuri!!
Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**
Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni
**01/01/2022 MPAKA 15/02/2022**
**Asante**
116653602




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Viongozi wa Afrika Magharibi wakutana baada ya mapinduzi

**Accra,** GHANA

MKUTANO muhimu wa viongozi wa Afrika Magharibi, umeanza katika mji mkuu wa Ghana, Accra, kufuatia mapinduzi kadhaa katika eneo hilo pamoja na hali mbaya ya ukosefu wa utulivu kutokana na ghasia za wanajihadi.

Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), imetuma wajumbe wawili Burkina Faso baada ya jeshi kunyakua mamlaka mwezi uliopita.

Umoja huo wenye wanachama 15, umesimamisha uanachama wa Burkina Faso.

Katika kipindi cha mwaka jana, ECOWAS, imeweka vikwazo kwa Mali na Guinea, kufuatia mapinduzi na viongozi wa kijeshi kusita kurejesha utawala wa kiraia.

Kinachoongeza msukosuko wa eneo hilo ni shambulio la bunduki siku ya Jumanne, kwa rais wa Guinea-Bissau, Umaro Sissoco Embalo.

Maofisa walielezea hilo kama jaribio la kunyakua madaraka.

**BBC**

# Mvuvi ajiokoa kwa kupigana na mamba

**Maputo,** MSUMBIJI

MTU mmoja amepigana vita vikali dhidi ya mamba katika harakati za kuokoa wavu wake wa kuvulia samaki.

Joao Armando,35, kwa sasa yuko hospitalini akiuguza jeraha akiwa katika hatari ya mkono wake mmoja kukatwa, baada ya mkono wake wa kushoto kuumwa na mamba huyo mkubwa, mguu wake wa kulia pia ulijeruhiwa.

Alikuwa akivua samaki katika mto Shire, ambao hupeleka maji yake katika mto Zambezi, wakati alipomuona mamba huyo anaukatakata wavu wake.

Akiwa ufukweni, alijaribu kuuvuta wavu huo, mamba huyo alimvuta ndani ya maji na hapo ndipo vita vikali vikaanza.

"Mamba huyo alinivamia, nikajaribu kumuua," alisema Armando kwa lugha ya Csena, inayozungumzwa eneo hilo.

Katika vita hivyo, mamba huyo alimuingiza mvuvi huyo ndani ya maji," nilipiga kelele kupata usaidizi na muda mfupi nikaokolewa na watu waliokuwa karibu."

Daktari wa upasuaji aliyemtibu alisema kwamba, alikuwa amepoteza fahamu alipowasili katika kliniki katika eneo la Mortumbala.

Armando alihamishwa katika hospitali nyingine katika mji wa Quelimane kwa matibabu zaidi.

**BBC**

# Adai kumtafuta Mungu kwa kuiba Biblia Kenya

**Nairobi,** KENYA

MWANAMUME ambaye amekamatwa na kushtakiwa kwa kuiba biblia mbili, kwenye duka kubwa jijini Nairobi, anasema alichokuwa akitaka ni kumjua Mungu tu.

Augustine Wanyonyi, 35, aliiambia mahakama kwamba aliiba Biblia hizo, ili asome na kumjua Mungu zaidi.

Alipoulizwa kwa nini aliiba nakala mbili badala ya moja, alisema Biblia ya pili alikusudia kwa ajili ya mkewe.

Wanyonyi alifika mbele ya Hakimu Mkuu wa mahakama ya Milimani katika Jiji la Nairobi, Susan Shitubi, alikiri kutenda kosa hilo.

"Niliiba biblia ili nisome, nielewe na kuhubiri neno la Mungu badala ya kujiua kutokana na matatizo yanayonikabili," Wanyonyi aliambia mahakama. Alishtakiwa Februari Mosi, mwaka huu na kurudi mahakamani kuhukumiwa baada ya kupatikana na hatia ya kosa hilo.

Wanyonyi, alikamatwa Jumapili baada ya kupatikana na nakala mbili za biblia zenye thamani ya shilingi 2,100 za Kenya.


Kulingana na ripoti ya polisi iliyosomwa na wakili wa serikali, Alice Mathangani, mshtakiwa alikwenda kwenye duka hilo mwendo wa saa tisa alasiri, katika tarehe iliyotajwa, na kuiba biblia hizo mbili na kuzificha ndani ya suruali yake.

"Alinaswa na kanda ya CCTV ya duka kuu na baadaye kukamatwa na wahudumu wa CCTV, baada ya kushindwa kulipia bidhaa sawa na hiyo alipofika kwa kaunta," mwendesha mashtaka alidai.

Mwendesha mashtaka pia aliiambia mahakama kuwa mshtakiwa alikuwa na rekodi ya awali ya wizi wa dukani, alishtakiwa Desemba mwaka 2021, akaachiliwa na mahakama nyingine baada ya kuomba msamaha.

Hakimu aliamuru ripoti ya kabla ya hukumu iwasilishwe mahakamani ndani ya siku saba.

Atafikishwa mahakamani kuhukumiwa Februari 16, mwaka huu. **BBC**



Watu wakikagua jengo lililoharibiwa baada ya shambulio lililofanywa na jeshi la Marekani, nchini Syrian katika kijiji cha Atmeh, **PICHA: AP**

# Radi yaua watu 26 DRC

**Kinshasa,** DRC

WATU 26 wamefariki dunia, baada ya radi kupiga katika waya unaobeba umeme mwingi katika vitongoji vya mji mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kinshasa, na kuangukia nyumba na soko, serikali imesema.

Shirika la habari la Reuters, limeripoti kwamba watu 24 waliofariki dunia walikuwa ni wanawake na wanaume wawili huku wengine wawili wakijeruhiwa vibaya, kwa mujibu wa ujumbe wa Twitter wa msemaji wa serikali ya Congo Patrick Muyaya.

Nyaya za umeme mara kwa mara, zimekuwa zikianguka jijini Kinshasa, mji wenye wakazi milioni 13 na ambao pia miundombinu yake imepitwa na wakati pamoja na kuwapo makazi ya watu yasiyo rasmi, hasa kwenye maeneo ambako hakujatengwa kuwa makazi ya watu.

Chama cha Wasanifu Majengo DRC, katika taarifa yake kuhusiana na ajali hiyo, kimesema vifo hivyo vingeepukika na ni kutokana na tukio la kutoheshimu kanuni za mipango miji kwenye njia za umeme mkubwa. **VOA**

# Uchunguzi waanza jaribio mapinduzi Guinea Bissau

**Bissau,** GUINEA BISSAU

SERIKALI ya Guinea Bissau, imeanzisha uchunguzi kuhusu jaribio la kumpindua Rais Umaro Sissoco Embalo, lililotokea siku ya Jumanne, jijini Bissau na kusababisha vifo vya watu 11.

Siku ya Jumanne, watu waliojihami kwa silaha, walivamia majengo ya serikali jijini Bissau, wakati rais Umaro Sissoco Embalo, alipokuwa katika kikao na mawaziri wake na kuanza kufyatua risasi.

Rais Embalo, mwenye umri wa miaka 49, alisema aliponea kuuawa au kujeruhiwa wakati wa makabiliano ya risasi yaliyodumu kwa saa tano, lengo kuiondoa serikali yake.

Msemaji wa Serikali, Fernando Vaz, alisema miongoni mwa watu 11 waliouawa ni pamoja na wanajeshi na raia wanne, akiwamo mtumishi wa serikali katika Wizara ya Afya pamoja na dereva wake.

Shughuli za kawaida zimeanza kurejea jijini Bissau, wakati huu taarifa za jeshi zikisema uchunguzi umeanza kubaini ukweli kuhusu tukio hilo katika nchi hiyo ya watu Milioni Mbili.

**RFI**

# AZAM FC, DODOMA JIJI TAMBO ZATAWALA BARA

**Na Saada Akida**

MBIO za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara zinatarajiwa kuendelea tena leo kwa 'Wanalambalamba' Azam FC kuwakaribisha Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Katika mchezo huo, Azam FC itaendelea kumkosa mshambuliaji wake, Iddi Seleman 'Nado' pamoja na Nicholas Wadada wakati Dodoma Jiji yenyewe itashuka dimbani bila ya nyota wake, Anuari Jabir ambaye amefungiwa michezo mitatu.

Kuelekea mchezo huo, makocha wa timu zote mbili wametamba wamejiandaa kuondoka na pointi tatu kwa ajili ya kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo ya juu nchini.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Azam FC, John Yona, alisema wamejiandaa kufanya vizuri katika mchezo huo ili kuendeleza rekodi ya kushinda waliyoianza hivi karibuni na kujiimarisha kwenye msimamo.

Yona alisema wanataka kufanya vyema kama kwenye mechi zilizopita na kwa sababu hiyo wanauona mchezo huo kama fainali ili wazibakishe pointi tatu nyumbani.

"Tumefanya maandalizi mazuri, tutahakikisha tunaendelea na kazi yetu ya kupata matokeo mazuri katika mchezo wetu dhidi ya Dodoma Jiji FC," alisema Yona.

Naye Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji FC, Renatus Shija, aliliambia gazeti hili mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu kutokana na ubora wa wapinzani wao.

Shija alisema wamejipanga kufuta makosa ya mchezo uliopita ambapo walipoteza dhidi ya Kagera, na sasa nguvu zao wanazihamishia kupata alama tatu muhimu katika mchezo huo.

"Kikosi chetu kipo vizuri na tumejipanga kuhakikisha tunapata alama muhimu ili kurejea nyumbani na pointi tatu, tunajua hautakuwa mchezo rahisi, hivyo tutapambana muda wote huku tukicheza kwa tahadhari," alisema Shija.

Aliongeza walikuwa na matatizo katika safu yao ya ulinzi lakini tayari imefanyiwa kazi ili kuhakikisha hawaruhusu washambuliaji wa Azam kutikisa nyavu zao.

Nahodha wa Dodoma Jiji FC, Emmanuel Martin, alisema wamepata maelekezo kutoka kwa kocha wao na kilichobakia ni kwenda kufanyia kazi uwanjani na hatimaye kuondoka na ushindi.

"Tumejiandaa vizuri, tunaenda kuonyesha ushindani kwa sababu tunajua Azam FC wanahitaji pointi tatu, na hata sisi tunazihitaji hizo, hivyo hatuendi kubutua tunatafuta matokeo na kucheza mchezo na kuwapa burudani wadau wa soka," alisema Martin.

## *JKU yaitambia Back Sailor*

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIKOSI cha JKU kimetamba kitaondoka na alama tatu katika mchezo wao wa kwanza wa mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Black Sailor utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

JKU inashuka dimbani ikiwa na alama 27 na iko katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi huku Black Sailor yenye pointi 19 iko katika nafasi ya 10.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa JKU, Sheha Khamisi, alisema wanaenda kuanza mzunguko mgumu ambao kila timu inahitaji kupata matokeo mazuri ili kuhakikishia wanafikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Sheha alisema wamejipanga vyema na anamatumaini makubwa ya kupata ushindi lakini wakiwaheshimu alama tatu hapo wapinzani wao nao watakuja na mbinu ili washinde kulingana na nafasi waliyoko katika msimamo wa ligi.

"Tumejiandaa kushindana, kupata alama tatu, kwa kuwa tunajua mzunguko huu kila mtu anataka kutimiza lengo lake hivyo na sisi ni miongoni kwa mwenye lengo la kutwaa taji la Ligi Kuu," alisema Sheha.

Wakati huo mechi kati ya Kisiwani dhidi ya Kipanga iliyopangwa kuchezwa leo imesogezwa mbele hadi keshokutwa kutokana na changamoto ya usafiri iliyoikumba Kipanga iliyotakiwa kusafiri kuelekea Pemba.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), walipokuwa wanapanda ndege kuelekea Ethiopia juzi kuwafuata wenyeji katika mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia (U-20) itakayochezwa leo nchini humo. **PICHA: TFF**

## Kili Marathon'22 usajili kufungwa

**Na Dennis Fusi**

HUKU zikiwa zimebaki takriban wiki tatu tu kabla ya kufanyika kwa mbio za 20 za Kilimanjaro Marathon 2022, waandaaji wa mbio hizo wamewakumbusha washiriki usajili utafungwa ifikapo Jumatatu.

Taarifa iliyotolewa jijini Dar es Salaam jana, ilisema baada ya usajili kufungwa, hakutakuwa na ruhusa ya kushiriki kwa wanariadha ambao hawakujisajili.

**"Usajili ni kwa njia ya mtandao kwa kupitia tovuti yetu ya www.kilimanjaromarathon.com au Tigo Pesa kwa kupiga *149*20#. Mtandao hautafanya kazi baada ya Februari 7, 2022 kwa hivyo ni bora watu watumie muda uliobaki kufanya usajili," ilisema taarifa ya waandaaji hao.**

Hata hivyo walisema usajili wa mbio za Grand Malt za Km 5 maarufu kama Fun Run utaendelea hata baada ya tarehe hiyo iliyotajwa na pia katika vituo kuchukulia namba za kukimbilia.

"Tunapenda pia kuwakumbusha washiriki kuwa endapo nafasi zitajaa kabla ya Februari 7, 2022 basi tutalazimika kufunga usajili mara moja, " iliongeza taarifa hiyo.

Wadhamini wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 ni Bia ya Kilimanjaro (Mdhamini Mkuu) Tigo (Kilomita 21) na Grand Malt wanaodhamini kilomita tano.

Katika hatua nyingine, kwa mara ya kwanza kutakuweko na maonyesho yanayojulikana kama Kili Expo ambapo wadhamini na wadau wengine wa mbio hizo watapata fursa ya siku tatu za kuonyesha bidhaa na huduma wanazotoa kuanzia Februari 24 hadi 26, mwaka huu.

Mbio za Kilimanjaro Marathon zitafanyika Februari 27, mwaka huu, katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na zimeandaliwa na Taasisi ya Kilimanjaro Company Limited na kuratibiwa na Executive Solutions.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO AICHOKA PSG

KOCHA wa PSG raia wa Argentina, Mauricio Pochettino, mwenye umri wa miaka 49 anasemekana kuchoshwa na ukosoaji ambao amevumilia katika mji mkuu wa Ufaransa, Paris, na hana nia ya kusalia na klabu hiyo zaidi ya msimu huu. **(Footmercato)**

### UNITED YAMTAKA POCHETTINO

KLABU ya Manchester United inazidi kujiamini inaweza kumteua Kocha wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino kama kocha wao wa kudumu katika majira ya joto. (**Mirror**)

### SILVA MAMBO SAFI

MANCHESTER City wako kwenye mazungumzo na kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva kuhusu mkataba mpya wa muda mrefu licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuwa tayari ana mkataba unaoendelea hadi mwaka 2025. (Times)

### MILITAO KUMRITHI RUDIGER

MLINZI wa kati wa Real Madrid, Eder Militao mwenye umri wa miaka 24 anasakwa na kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel msimu wa joto kama mbadala wa Mjerumani, Antonio Rudiger (28). **(AS)**

### ARSENAL YAIGOMEA PALACE

OMBI la pili la Crystal Palace la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah limekataliwa, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 raia wa England kubakia na miezi sita kwenye mkataba wake. (**Sky Sports**)

### RAPHINHA SOKONI

KLABU ya Chelsea imewasilisha ombi la kutaka kumsajili winga wa Leeds na Brazil Raphinha, lakini huenda mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 akapatikana katika dirisha la uhamisho la msimu wa joto.(**Daily Mail**)

### ZAKARIA KUTUA JUVE

KIUNGO wa kati wa Uswisi, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 25, anaelekea kujiunga na Juventus baada ya klabu hiyo ya Italia kukubali mkataba na Borussia Monchengladbach. (**Goal**)

### BISSOUMA NJIA MOJA

KIUNGO wa kati wa Mali na Brighton, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 25, huenda akaondoka Aston Villa, huku Tottenham na Manchester United wakiwa na nia ya kumsajili. (**Journalist**)

### LACAZETTE ANUKIA LYON

RAIS wa Lyon, Jean-Michel Aulas amesema klabu hiyo itafanya kila iwezalo kumsajili tena mshambuliaji wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 30, Alexandre Lacazette kutoka Arsenal msimu wa joto. (**Sun**)

### SPURS, JUVE VITANI

TOTTENHAM Hotpurs na Juventus zote zinavutiwa na winga wa Roma mwenye umri wa miaka 22, Nicolo Zaniolo. (**Calciomercato**)

### SALIBA AGOMBEWA ULAYA

MABINGWA wa Italia, Inter Milan na wapinzani wao wa jiji la AC Milan wako tayari kumenyana na Real Madrid katika usajili wa beki wa kati wa Arsenal wa chini ya miaka 21, William Saliba mwenye miaka 20. (**Calciomercato**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANE: HAIKUWA RAHISI KUTINGA FAINALI AFCON

Afunguka walifahamu ugumu wa mechi hiyo lakini Senegal walionyesha...

**YAOUNDE, Cameroon**

SADIO Mane amesema Senegal kutinga fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), haikuwa rahisi kwa sababu Burkina Faso walionyesha upinzani mkubwa na waliwapa wakati mgumu.Mane alifunga bao la tatu kwenye mchezo wa nusu fainali dhidi ya Burkina Faso na kuiwezesha Senegal kuibuka na ushindi wa magoli 3-1, hapo juzi.

Licha ya Senegal kukataliwa penalti mbili na VAR, lakini dakika 30 za mwisho za mchezo huo zilionekana kuwa bora zaidi kwao.

Abdou Diallo na Idrissa Gueye waliiweka mbele Senegal kwa mabao mawili kabla ya Blati Toure kufunga moja kwa Burkina Faso.

**Lakini Mane aliwazidi akili mabeki wa Burkina Faso na kuuwahi mpira na kufunga bao la tatu kwa Senegal na kuwahakikishia kutinga fainali ya michuano hiyo.**

Hilo lilikuwa bao la 29 kwa Mane kuifungia timu ya taifa, na kumfanya kuwa sawa na Henri Camara katika orodha ya wafungaji bora wa wakati wote wa nchi hiyo.

"Ilionyesha namna gani tuna nguvu," alisema Mane akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Tulijua haungekuwa mchezo rahisi kutinga fainali ya AFCON kwa mara ya pili mfululizo.

"Lakini jambo la muhimu zaidi kwetu ni kufuzu kwa fainali na hatujali nani tutakayekabiliana naye.

"Tulicheza dhidi ya timu ngumu sana Burkina Faso ambao walitupa wakati mgumu sana.

"Tulitarajia kuwa na mchezo mgumu, lakini tulitulia na kutengeneza nafasi nyingi. Nafikiri tulistahili ushindi."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 896

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
MIDDLESBROUGH
1 | 1.38
X | 4.59
2 | 7.52

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NDOMBELE: NILIHITAJI KUONDOKA TOTTENHAM



**PARIS, Ufaransa**

TANGUY Ndombele amekubali alipata msongo wa mawazo akiwa kwenye klabu ya Tottenham Hotspur baada ya kuwa chini ya makocha watano huku akiwa hana mwendelezo wowote na hakuhitaji kuona mwisho wake ukiwa ndani ya klabu hiyo.

Ndombele alieleza jinsi ambavyo hali hiyo ilimuathiri kwa kutokuwa na mwendelezo mzuri baada ya klabu hiyo kuwa chini ya makocha watano ambao ni pamoja na Mauricio Pochettino, Jose Mourinho, Ryan Mason, Nuno Espirito Santo na Antonio Conte.

"Halikuwa kosa lao lakini nilikuwa na tatizo kidogo nikiwa Tottenham, nilikuwa nataka kitu kingine zaidi," alisema Ndombele mara baada ya kukamilisha usajili wa kutua Lyon.

Alipohojiwa na kituo cha RMC Sport, alinukuliwa akisema, "Sikusita klabu ya Lyon ilipoonyesha nia ya kunihitaji, mazungumzo yalikuwa haraka, nina furaha kurudi, najua Lyon ni wazuri kuendana na mazingira, nina miezi mitatu na nusu kabla ya msimu kuisha, Lyon sio sehemu mbaya kwangu."

Ndombele alivunja rekodi ya usajili kwenye klabu ya Tottenham mwaka 2019, lakini hakuwa na wakati mzuri kwenye kikosi cha timu hiyo, katika misimu miwili na nusu aliyoitumikia klabuni hapo.



# Costa awa mchezaji huru

**MADRID, Hispania**

DIEGO Costa kwa sasa anapatikana kwa uhamisho baada ya kuondoka Atletico Mineiro ya Brazil mwezi uliopita ambako alikuwa akilipwa mshahara wa pauni 46,000 kwa wiki.

Costa nyota wa zamani wa Chelsea mwenye umri wa miaka 33, inasemekana alipewa ofa kwenda klabu ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Mainz lakini alikataa.

Kwa mujibu wa gazeti la Bild, mshauri wa Mainz alipongeza huduma ya mshambuliaji huyo kwa kutuma ujumbe kwa mmoja wa maskauti wao kwenye WhatsApp.

Taarifa inataja Costa alitaka mkataba wa miezi 18, lakini skauti wake hakuichukulia ofa hiyo kwa uzito mkubwa.

Suala hilo lilifanya taarifa sahihi juu ya uwezekano wa dili hilo kutomfikia Mkurugenzi, Martin Schmidt kwa wakati, kutokana na dau alilotaja Costa. Zaidi inadaiwa mkurugenzi naye alipoambiwa baadaye akasema hata angekuwa yeye asingeamini uzito wa ofa hiyo.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, klabu ingeweza kumlipa takribani euro milioni nne kwa mwaka kama alivyotaka.

Barcelona na Arsenal wanatajwa walikuwa kwenye hatua za kufanya uamuzi juu ya nyota huyu pia.

Rafiki yake John Terry anashindwa kuamini Costa amekosa klabu hadi sasa, lakini inatajwa kwamba, Fenerbahce inamtaka.

## HABARI MICHEZO

,686,220

# POLISI TANZANIA YAZINDUA 'UTATOA HUTOI' KUJIINUA

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Maafande wa Polisi Tanzania kimekuja na kauli mbiu ya 'Utatoa Hutoi' na wako tayari kusaka pointi tatu katika mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu mkoani Geira, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alisema kikosi chake kipo safarini kuelekea Geita kwa ajili ya ya mchezo huo na wanakwenda huko kwa kazi moja ya kuchukua pointi zote kutoka kwa wenyeji wao.

Malale alisema wanaenda Geita kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu wenyeji wao wanarekodi nzuri wanapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani.

"Katika michezo mitano ya hivi karibuni hatujakupata matokeo ya ushindi zaidi ya sare nne, miwili nyumbani na ugenini na kupoteza dhidi ya Yanga."

"Tulirejea uwanjani kufanyia kazi madhaifu yetu na sasa tuko vizuri kwa ajili ya mchezo dhidi ya Geita Gold FC, nina imani kwetu utakuwa ni fainali ili kurejea katika kasi yetu tuliyoanza nayo msimu huu," alisema Malale.

Baada ya mchezo huo, Polisi Tanzania itasafiri tena kuelekea Tanga kuwafuata Coastal Union kwa ajili ya mchezo mwingine wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa Februari 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini humo.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wenye Ulemavu ya kurusha tufe, Sauda Njopeka (kushoto) na Ignas Mtweve, wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Jumuiya ya Madola yatakayofanyika Julai, mwaka huu nchini Uingereza. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TFF yafurahia ushindani FA

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limepongeza ubora na ushindani uliooko katika mashindano ya Kombe la FA ambayo hutoa mwakilishi wa Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, likisema timu nyingi kwa sasa hazifanyi mzaha kwenye michuano hiyo tofauti na zamani.

Mkurugenzi wa Mashindano wa TFF, Salum Madadi, alisema pamoja na hayo, michuano hiyo msimu huu imeonyesha timu za Ligi Kuu Tanzania Bara kupiga hatua kubwa kiuwezo, ikionyesha dhahiri ubora wa ligi yenyewe.

"Kwanza nichukue fursa hii kuzipa pole timu za Daraja la Kwanza kwa kukutana na vipigo vizito, maana kuna jamaa wamepigwa nane na wengine sita, lakini nazipongeza kwa sababu mpaka kufikia pale zimefanya kazi kubwa, hivyo zisikate tamaa, " alisema Madadi.

Aliongeza kwa sasa inaonyesha Ligi Kuu Tanzania Bara ni bora sana, kwani uwezo wa timu zake unaonekana ukilinganisha na timu za chini, wakati miaka ya nyuma zilikuwa hazitofautiani sana.

"Huko nyuma timu za Ligi Kuu na madaraja ya chini zilikuwa zikizidiana kwa madaraja, lakini viwango vilikuwa havipishani sana na hata ushindani wa uwanjani ulikuwa haupishani, lakini ubora wa ligi umezifanya timu kupiga hatua kubwa, pia zinaonekana hazifanyi mzaha kwenye kombe hili," alisema.

Timu zilizobebeshwa mabao mengi kwenye michuano hiyo ya FA ni Top Boys, iliyobugizwa mabao 8-1 dhidi ya Coastal Union, huku Dar City, ikikandamizwa mabao 6-0 dhidi ya Simba kwenye hatua hiyo ya 32 bora.

## JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/02/22 | 18:00 | Hull City vs Preston | 2.55 | 3.25 | 2.80 |
| 02. 05/02/22 | 18:30 | Maritimo vs GD Estoril | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 05/02/22 | 19:00 | St Etienne vs Montpellier | 2.57 | 3.31 | 2.67 |
| 04. 05/02/22 | 20:30 | Swansea vs Blackburn | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 05. 05/02/22 | 21:00 | Pacos Ferreira vs Portimonense | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 06. 05/02/22 | 23:00 | Twente vs Vitesse Arnhem | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 07. 06/02/22 | 16:00 | Valencia vs Real Sociedad | 2.70 | 3.20 | 2.65 |
| 08. 06/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Galatasaray | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 09. 06/02/22 | 16:00 | Amorebieta vs Real Oviedo | 2.79 | 3.04 | 2.55 |
| 10. 06/02/22 | 17:00 | Sampdoria vs Sassuolo | 2.81 | 3.56 | 2.36 |
| 11. 06/02/22 | 18:15 | Barcelona vs Atletico Madrid | 2.40 | 3.26 | 2.97 |
| 12. 06/02/22 | 20:00 | Udinese vs Torino | 2.86 | 3.21 | 2.51 |
| 13. 06/02/22 | 20:30 | Betis vs Villarreal | 2.33 | 3.44 | 2.94 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 04/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2316 | Hilal Al-Quds vs Tubas | 1.41 | 4.24 | 6.55 |
| 16:00 | 3209 | Nkwazi vs Prison Leopards | 2.22 | 2.85 | 3.90 |
| 16:00 | 4907 | Adama City FC vs Ethiopia Bunna SC | 3.80 | 2.94 | 2.01 |
| 16:30 | 1101 | Cagliari Youth vs Empoli Youth | 2.31 | 3.05 | 2.95 |
| 16:30 | 3971 | Inter Youth vs Sampdoria Youth | 1.92 | 3.77 | 3.19 |
| 16:30 | 4431 | Havadar vs Esteghlal Tehran | 5.80 | 3.00 | 1.80 |
| 16:35 | 2812 | Al Arabi Doha SC vs Al-Shamal | 1.45 | 4.43 | 5.39 |
| 16:35 | 5620 | Al Ahli Doha SC vs Al Khoor | 1.86 | 3.56 | 3.56 |
| 18:30 | 5714 | CS Mioveni vs Voluntari | 2.65 | 2.90 | 2.80 |
| 18:45 | 2826 | Umm-Salal SC vs Qatar SC | 2.50 | 3.32 | 2.50 |
| 19:00 | 1064 | Azam vs Dodoma FC | 1.73 | 3.19 | 4.83 |
| 19:00 | 1393 | Wolfsberger AC vs Floridsdorfer AC | 1.25 | 5.40 | 8.49 |
| 20:00 | 1463 | Nieciecza KS vs Jagiellonia | 2.84 | 3.22 | 2.29 |
| 20:00 | 2556 | Slaven Belupo vs HNK Sibenik | 1.90 | 3.37 | 3.61 |
| 20:00 | 2622 | Kayserispor vs Hatayspor | 2.33 | 3.25 | 2.96 |
| 20:00 | 3011 | Konyaspor vs Giresunspor | 1.98 | 3.26 | 3.81 |
| 20:30 | 2113 | Heidenheim vs Hannover | 2.12 | 3.29 | 3.29 |
| 20:30 | 5318 | Nurnberg vs Ingolstadt | 1.67 | 3.73 | 4.71 |
| 21:00 | 2345 | Laval vs Bastia Borgo | 1.67 | 3.66 | 4.69 |
| 21:00 | 3001 | Red Star vs Saint Brieuc | 2.03 | 3.22 | 3.56 |
| 21:00 | 4202 | Chateauroux vs Creteil | 1.69 | 3.53 | 4.80 |
| 21:00 | 4234 | Sete 34 FC vs Le Mans | 2.86 | 3.01 | 2.48 |
| 21:00 | 4499 | Chambly vs Orleans | 2.78 | 3.18 | 2.43 |
| 21:00 | 4843 | Freiburg II vs Viktoria Koln | 2.49 | 3.13 | 2.79 |
| 21:00 | 5127 | Benfica Lisbon B vs Casa Pia Atletico | 2.33 | 3.23 | 2.89 |
| 21:00 | 5287 | Boulogne vs Annecy FC | 3.27 | 3.08 | 2.20 |
| 21:00 | 5406 | Sedan vs Cholet | 2.16 | 3.22 | 3.22 |
| 21:00 | 5908 | Bourg Peronnas vs Avranches | 1.69 | 3.67 | 4.50 |
| 21:20 | 2314 | Josko Ried vs Austria Klagenfurt | 2.16 | 3.37 | 2.94 |
| 21:30 | 5553 | Neuchatel Xamax vs FC Schaffhausen | 2.31 | 3.37 | 2.70 |
| 22:00 | 1218 | Jong PSV vs Helmond Sport | 1.52 | 4.11 | 5.48 |
| 22:00 | 1826 | Telstar vs De Graafschap | 4.58 | 3.80 | 1.66 |
| 22:00 | 1974 | FC Volendam vs Jong Utrecht | 1.25 | 5.84 | 8.56 |
| 22:00 | 2342 | Dordrecht vs Almere City | 3.56 | 3.66 | 1.88 |
| 22:00 | 2392 | Jong Ajax vs Jong AZ Alkmaar | 1.50 | 4.49 | 5.08 |
| 22:00 | 2753 | NAC Breda vs Roda Kerkrade | 2.64 | 3.37 | 2.44 |
| 22:00 | 3717 | Maastricht vs VVV Venlo | 3.28 | 3.47 | 2.03 |
| 22:00 | 3980 | Emmen vs FC Oss | 1.42 | 4.57 | 6.22 |
| 22:15 | 5847 | FC Vaduz vs FC Winterthur | 2.35 | 3.46 | 2.60 |
| 22:30 | 1231 | Zaglebie Lubin vs Legia Warszawa | 3.47 | 3.38 | 1.94 |
| 22:30 | 2170 | Hertha BSC vs VfL Bochum | 2.20 | 3.38 | 3.18 |
| 22:45 | 3098 | Charleroi vs RFC Seraing | 1.71 | 3.91 | 4.26 |
| 22:45 | 3726 | Birmingham vs Sheffield Utd | 3.43 | 3.28 | 2.07 |
| 22:45 | 5548 | Arbroath vs Kilmarnock | 2.69 | 3.13 | 2.54 |
| 23:00 | 1354 | Burgos vs Alcorcon | 1.86 | 3.28 | 4.21 |
| 23:00 | 1554 | Llagostera vs Villarreal B | 3.42 | 3.27 | 1.99 |
| 23:00 | 2149 | Manchester Utd vs Middlesbrough | 1.38 | 4.59 | 7.52 |
| 23:00 | 4053 | Marseille vs Angers | 1.52 | 4.19 | 5.99 |
| 23:00 | 5157 | Almeria vs UD Ibiza Eivissa | 1.86 | 3.34 | 4.13 |
| 23:00 | 5426 | Getafe vs Levante | 2.00 | 3.10 | 4.20 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Februari 4, 2022

Nipashe




Mane: Haikuwa rahisi kutinga fainali AFCON

UKURASA 21

# Yanga yaitisha Mbeya City FC

## ●●● Yawataka wajiandae kusulubiwa kwa sababu hawataki kuharibu...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU wakiwa na rekodi ya kutopoteza mechi, Yanga ya jijini Dar es Salaam imesema haina hofu ya kukutana na timu yoyote katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ambayo hivi sasa imeingia kwenye raundi ya 14.

Yanga ambao ndio vinara wanajiandaa kuikaribisha Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Hata hivyo taarifa zilizolifikia gazeti hili zinasema huenda wachezaji wake wawili, Feisal Salum 'Fei Toto' na Dennis Nkane wakakosekana katika mechi hiyo kwa sababu hawako fiti.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema jana wamejiandaa kushinda mechi hiyo kutokana na ubora wa kikosi chao kwa sasa, na kamwe hawawahofii Mbeya City ambayo iliwafunga Simba ilipowafuata Mbeya.

Bumbuli alisema Yanga imeimarika na imejipanga kuhakikisha msimu huu inafikia malengo yake, hivyo kila mechi kwao ni zaidi ya fainali.

Alisema timu yake imeshacheza mechi ngumu zaidi kwenye ligi msimu huu na walifanikiwa kuvuka vikwazo hivyo, kwa hiyo wanaikaribisha Mbeya City kama walivyozipokea timu nyingine.

"Tunakwenda kukutana na Mbeya City iliyoimarika msimu huu, hatuwaogopi, na wala hawatuogopi matokeo waliyoyapata kwa sababu kila mtu ana uzuri wake na ubora wake.Walikutana na timu isiyokuwa bora , wao wakawa bora zaidi yao wakashinda, wanakuja kukutana na sisi ambao tuna ubora mkubwa zaidi," alisema Bumbuli.

Aliongeza Yanga ya sasa haijifichi na ndiyo sababu haijapoteza mechi yoyote ile kutokana na kusukwa na kikosi bora na kilichojipanga kuchukua ubingwa msimu huu na si vinginevyo.

"Tukiwa na chagizo la kupita katika mtihani wa mechi ngumu zaidi ya hii, ndiyo maana tunakwenda kucheza Uwanja wa Benjamin Mkapa mechi yetu ya Jumamosi tukiwa tunajiamini, tutahakikisha tunapata pointi tatu ili tuzidi kujiimarisha," Bumbuli alisema.

Aliongeza mchezo huo utakuwa muhimu kwao katika kuendelea na mbio za kuwania ubingwa kwa kukusanya pointi zote tatu, kwani kitendo chochote kile cha kudondosha kitawaweka katika mazingira magumu.

"Ukiwa katika mbio za ubingwa unatakiwa kukusanya pointi tatu kwenye mechi nyingi, lakini ukiwa unaangusha pointi mara kwa mara, mbili au tatu, kidogo unajiweka kwenye mazingira magumu, sisi tunalijua hilo," Bumbuli aliongeza.

Alisema katika mechi ya kesho kuna hatihati ya kumkosa Fei Toto na Nkane ambao kiafya wana changamoto.

"Hawa walikuwa majeruhi na wameanza mazoezi mepesi, sasa leo (jana) na kesho (leo) watakuwa vipi kiafya, bado ni hatihati, kama wakiwa vyema na kuunganishwa kwenye kikosi watacheza, lakini kama hawatakuwa na utimamu wa mwili mzuri kwa ajili ya mechi hiyo, basi watasubiri mechi zijazo," aliongeza ofisa huyo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mbeya City ina pointi 22 na iko katika nafasi ya tatu huku mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 25 wakiwa nafasi ya pili.

Baada ya mechi hiyo, Mbeya City ambayo ilishaondolewa kwenye michuano ya Kombe la FA, itasafiri kuwafuata Namungo katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Februari 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi.




Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Senzo Mbatha (kulia), akitoa mada katika semina elekezi iliyoandaliwa na klabu hiyo kwa kuhusisha benchi la ufundi pamoja na wachezaji kwa ajili ya kuhakikisha wanajiendesha kisasa na kufikia malengo yao katika msimu huu wa 2021/22. **PICHA: MTANDAO**

# Tanzanite katika mtihani Ethiopia

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens) inatarajia kuwakabili wenyeji Ethiopia katika mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia utakaochezwa leo jijini Addis Ababa.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar, Tanzanite Queens ilipata ushindi wa bao 1-0.

Mshindi wa jumla wa mechi hiyo atakutana kati ya Ghana au Uganda, mechi ya kwanza Ghana ikiwa ugenini ilipata ushindi wa mabao 2-1.

Kocha Mkuu wa Tanzanite Queens, Bakari Shime, alisema kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo na wamejipanga kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Shime alisema mchezo utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa kwa sababu ya uimara na ubora wa wapinzani wao lakini wao wamekwenda Ethiopia kutafuta ushindi na hatimaye kusonga mbele.

"Tumefanya maandalizi mazuri dhidi ya Ethiopia, wapinzani wetu wako vizuri kila idara, tumefanyia kazi ubora wao na kikosi kipo tayari kwa ajili ya kupambana ili kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wetu huo wa kesho (leo)," alisema Shime.

Aliongeza licha ya kuwa mbele dhidi ya wapinzani wao, anafurahi kuona wachezaji wake wana morali nzuri na kila mmoja amejiandaa kuhakikisha tunashinda na tunatimiza ndoto ya kwenda kwenye fainali za dunia.

Tanzanite Queens imefika raundi ya nne ya michuano hiyo ambayo fainali zake zitachezwa baadaye mwaka huu nchini Costa Rica baada ya kuwaondoka Eritrea na Burundi.

Ili kujiandaa na mchezo huo wa marudiano, Tanzanite Queens ilikwenda kuweka kambi Karatu, kwa ajili ya kuzoea hali ya hewa inayofanana na Addis Ababa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >